# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

آياتها ١٢٣ (١١) سُورَةُ هُودٍ مَكِّيَّةٌ (٥٢) ركوعاتها ١٠

*Ina Aya 123*

# SURAT HUD

*(Imeteremka Makka)*

*Ina Makara 10*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye hikima na Mwenye ujuzi wa kila kitu

الٓرٰ كِتَٰبٌ أُحْكِمَتْ ءَايَٰتُهُۥ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِن لَّدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ ①

2. (Imefanywa hivi) ili msiabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi kwenu ni muonyaji na mtoaji wa khabari njema ninayetoka kwake

أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّا ٱللَّهَ ۚ إِنَّنِى لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ ②

3. Na ili muombe msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie (mrejee) Kwake. Atakustarehesheni kwa starehe nzuri mpaka muda maalumu (mtapoondoka ulimwenguni). Na atampa (Akhera) kila mwenye fadhila, fadhila yake. Na kama mtakengeuka basi nakukhofieni adhabu ya (hiyo) siku kubwa.

وَأَنِ ٱسْتَغْفِرُوا۟ رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوٓا۟ إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُم مَّتَٰعًا حَسَنًا إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِى فَضْلٍ فَضْلَهُۥ ۖ وَإِن تَوَلَّوْا۟ فَإِنِّىٓ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ ③

4. Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu. Naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

إِلَى ٱللَّهِ مَرْجِعُكُمْ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ④

5. Sikilizeni! Wao wanaficha vilivyo vifuani mwao ili wamfiche Mwenyezi Mungu (asiwatambue). Sikilizeni! Wanapojigubika nguo zao naye anajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Hakika Yeye ni Mjuzi wa (hata) yaliyomo vifuani.

أَلَآ إِنَّهُمْ يَثْنُونَ صُدُورَهُمْ لِيَسْتَخْفُوا۟ مِنْهُ ۚ أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ۚ إِنَّهُۥ عَلِيمٌۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ ⑤

6. Na hakuna nyama yoyote (yaani kiumbe chochote) katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu. Na anajua makao yake ya milele na mahali pake pa kupita tu. (Napo ni hapa duniani). Yote yamo katika Kitabu kinachodhihirisha (kila kitu. Kitabu chake Mwenyezi Mungu anachokijua Mwenyewe hakika yake, si kama vitabu tunavyovijua sisi).

وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۚ كُلٌّ فِى كِتَٰبٍ مُّبِينٍ ⑥

---

3. Kutubia ni kurejea. Na kurejea kwa Mwenyezi Mungu ni kujiepusha na makatazo Yake na kufanya maamrisho Yake. Na imetajwa jaza utakayoipata duniani na Akhera kwa kufanya haya.

6. Muradi wa neno hili "Riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu" ni kuwa Mwenyezi Mungu amekipa kila kitu ujuzi wa kujitafutia riziki yake kama alivyosema katia Aya ya 2 na ya 3 za *Suratul A'laa* kuwa: "Aliyeumba kila kitu na akakitengeneza. Na akakidiria (kila kimoja jambo lake; na akiongoza (kufanya jambo hilo)." Na akasema vile vile katika Aya ya 20 ya *Surat Abasa* "Kisha akamfanyia njia nyepesi (ya kufanya mambo yake)."

**7. Na yeye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi kwa siku sita. Na Arshi yake ilikuwa juu ya maji. (Kakuumbeni) ili kukufanyieni mtihani (aonyeshe) ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri (na nani mwenye vitendo vibaya). Na kama ukisema: "Nyinyi mtafufuliwa baada ya kufa," wale waliokufuru husema: "Hayakuwa haya (unayoyasema) ila ni udanganyifu waziwazi."**

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ
أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ
أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَلَئِن قُلْتَ إِنَّكُم مَّبْعُوثُونَ مِن
بَعْدِ الْمَوْتِ لَيَقُولَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَٰذَا
إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾

---

Na akataja katika Aya ya 68 ya *Suratin Nahl* (Sura ya kutaja habari ya nyuki) namna alivyomfahamisha Mwenyezi Mungu kufanya hayo anayoyafanya.

Na akawaambia Wànaadamu katika Aya ya 15 ya *Suratil Mulk:* "Yeye ndiye aliyefanya ardhi iwe inaweza kutumika kwa kila myatakayo kwa ajili yenu. Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika riziki zake".

Na anasema vile vile Mwenyezi Mungu katika Aya ya 10 ya *Suratil Jumua:* "Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi (ili msipate kufanya mabaya) ili mpate kufaulu." Sio kuongea misikitini.

Basi haya maneno ya Mwenyezi Mungu yanaonyesha wazi wazi kuwa watu wapige mbio wende huku na huku kutafuta riziki. Sio kupwetekea na kufunga mikono wakakaa kungojea kuruzukiwa vivi hivi, nao wamekaa kiwetewete.

Sio huo Uislamu kabisa. Uislamu hausemi hivyo kabisa. Bali unapinga kweli kweli uzembe huo. Unaupinga kwa maneno na vitendo. Maneno tumeona ya Mwenyezi Mungu haya.

Na yako mengi kabisa ya Mtume yanayohimiza haya ya kufanya kazi. Alisema "Hakupata kula mtu yoyote yule chakula chochote kile kilicho bora zaidi kuliko alichokichuma kwa mkono wake," sio kwa kugaiwa sadaka. Na amesema "Mkono wa juu (wa kutoa) ndio bora kuliko mkono wa chini (wa kupokea)." Na amesema "Mfanyaji biashara muaminifu (siku ya Kiama) atakuwa pamoja na Mitume na Siddiqina na Shuhadai."

Na katika kusifu Mtume mambo mazuri ya Uislamu alisema "Kazi ya mtu kuifanya kwa mkono wake (ajipatie riziki yake) na kila biashara isiyokuwa na kudanganya."

Na amesema: "Sehemu 9 katika sehemu 10 za riziki zinapatikana katika biashara na ukulima." Na vile vile amesema: "Mwenyezi Mungu anapenda kumuona mja wake (anarejea nyumbani kwake au katika nchi yake) na hali ya kuwa amechoka kwa kazi alizozifanya kwa ajili ya kutafuta riziki ya halali."

Na amesema: "Kuna katika madhambi dhambi ambazo hazifutwi ila kwa kutaabika katika kutafuta riziki." Na kuna chungu ya Hadithi za Mtume zinazosema namna hivi.

Bali mwenyewe Mtume (s.a.w.) hakukaa bure tangu utotoni mwake mpaka kufa kwake. Alipokuwa mdogo akichunga mbuzi wa watu kwa ijara. Aliponyanyuka kidogo alifanya vibiashara vidogo vidogo peke yake. Kisha akaongezea biashara yake, akatafuta wenziwe kuwa washirika wake. Miongoni mwa washirika wake hao alikuwa: Bwana Assaib bin Abis-Saib Al Makhzumy. Ambaye mwishoe alisilimu na akaishi muda mrefu katika Uislamu.

Na baadaye Mtume akatoka na biashara zake mwenyewe nje ya Makka. Na mwisho akatoka na biashara kubwa za Bibi Khadija kupeleka Shamu na kwengineko.

Na Masahaba pia, wote walikuwa wakifanya kazi. Ima kazi kubwa kubwa au ndogo ndogo au vijidogodogo kwa kiasi cha uweza wao. Masahaba 4 wakubwa kabisa hawa kazi zao zilikuwa hivi: Sayyidna Abubakrinis Siddiq: Mfanyi biashara kubwa ya nguo; Sayyidna Umar bin Khattab; Dalali; Sayyidna Uthman bin Affan: Mfanyaji biashara kubwa ya vyakula; Sayyidna Ali bin Abi Talib: Kazi ndogo ndogo hata za kuteka maji na kuuza majani.

Hakuna aliyejikalia bure.

Amesema Bwana mkubwa Sayyidna Umar bin Al Khattab: "Asijipwetekeze mtu akaacha kutafuta riziki akawa anaomba tu na kusema Ee Mola wangu! Niruzuku. Na hali ya kuwa anajua kuwa mbingu hazinyeshi dhahabu wala fedha. Na Mwenyezi Mungu anawaruzuku watu kwa kuamiliana wenyewe kwa wenyewe."

7. Na kusema kuwa Mbingu na Ardhi zimeumbwa kwa siku sita, anajua Mwenyewe Mwenyezi Mungu siku sita hizo ndio muda gani kwa hisabu yake Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Na hiyo ARSHI ya Mwenyezi Mungu pia hatujui wala MAJI hayo ambayo Arshi ilikuwa juu yake. ARSHI ni kitu alichojinasibishia Mwenyezi Mungu akasema kuwa yuko katika Arshi yake. Basi kama tusivyoijua hakika ya Mwenyezi Mungu ndivyo tusivyojua Arshi yake na kila kitu chake alichojinasibishia Mwenyewe Nafsi yake.

Kila inavyokupitia moyoni mwako kumshabihisha Mwenyezi Mungu basi sivyo. Vitu vilivyohusiana na Roho tu

8. Na kama tukiwakawishia (kuwaletea) adhabu mpaka muda uliokwishakuhisabiwa (na sisi kuwa tutawaadhibu katika muda huo) wanasema (kwa kejeli): "Ni nini kinachoizuia adhabu hiyo (isije)?" Sikilizeni! Siku itakapowajia haitaondolewa kwao, na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

وَلَئِنْ أَخَّرْنَا عَنْهُمُ الْعَذَابَ إِلَىٰ أُمَّةٍ مَّعْدُودَةٍ
لَّيَقُولُنَّ مَا يَحْبِسُهُ ۗ أَلَا يَوْمَ يَأْتِيهِمْ لَيْسَ
مَصْرُوفًا عَنْهُمْ وَحَاقَ بِهِم مَّا كَانُوا
بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٨﴾ ع

9. Na kama tukimuonjesha mwanadamu rehema inayotokana nasi; kisha tukaiondoa kwake, mara moja anakuwa mwenye kukata temaa kabisa na asiyekuwa na shukurani.

وَلَئِنْ أَذَقْنَا الْإِنسَانَ مِنَّا رَحْمَةً ثُمَّ نَزَعْنَاهَا مِنْهُ
إِنَّهُ لَيَئُوسٌ كَفُورٌ ﴿٩﴾

10. Na kama tukimuonjesha neema baada ya dhara iliyompata mara husema: "Taabu zimekwisha ondoka kwangu." (Wala hashughulikii kufanya mema wala kumshukuru Mwenyezi Mungu). Basi huwa (sasa) ni mwenye kufurahi sana (na) mwenye kujivuna kabisa

وَلَئِنْ أَذَقْنَاهُ نَعْمَاءَ بَعْدَ ضَرَّاءَ مَسَّتْهُ لَيَقُولَنَّ
ذَهَبَ السَّيِّئَاتُ عَنِّي ۚ إِنَّهُ لَفَرِحٌ فَخُورٌ ﴿١٠﴾

11. Lakini wale wanaosubiri na kufanya vitendo vizuri, hao ndio watakaopata msamaha na ujira mkubwa (kwa Mwenyezi Mungu kwani hawafanyi haya).

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ
لَهُم مَّغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١١﴾

12. Basi labda utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako (uliyoletewa Wahyi), na kifua chako kitaona dhiki kwa hayo, kwa sababu wanasema: "Mbona hakuteremshiwa khazina au kuja Malaika pamoja naye?" Wewe ni Muonyaji tu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa kila kitu.

فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَضَائِقٌ
بِهِ صَدْرُكَ أَن يَقُولُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ كَنزٌ
أَوْ جَاءَ مَعَهُ مَلَكٌ ۚ إِنَّمَا أَنتَ نَذِيرٌ ۚ وَاللَّهُ عَلَىٰ
كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٢﴾

---

hatuwezi kuvijua, seuze vilivyokhusiana na Mwenyezi Mungu. Anaambiwa Mtume: "Wanakuuliza hakika ya roho. Waambie kuwa Roho ni katika mambo ya (Mwenyewe Mwenyezi Mungu) Mola wangu. (Hayajui ila yeye Mwenyewe. Hayo muhali kujulikana). Hamkupewa nyinyi katika ujuzi ila sehemu ndogo tu."

Amesema Mwenyezi Mungu "Mwenye vitendo vizuri" hakusema Mwenye vitendo vingi, kuonyesha kuwa Wingi usiokuwa mzuri hauna maana. Kichache kizuri bora kuliko kingi kibaya.

Na sasa hizo amali za Uzushi ndio Zilizojaa na ndizo Zinazovaliwa Mbega na Kufungiwa Njuga. Kama mambo ya (a) Kuomba makaburini na (b) Kuyajenga na (c) Kuyawashia taa na (d) Kuyafanyia misikiti na (e) Kuyafanya ndio misikiti na (f) Maarubaini (g) na Matahalili (h) na Matanga ya siku za maziko na (i) ya ukumbusho wake kila mwaka na kama haya "Amewazainishia (amewapambia) Shetani amali zao (mbovu wakaziona nzuri) akawazuilia (kufuata) njia (aliyokuja nayo Mtume)." Kwa hivyo hawaongoki. "Na wakiambiwa Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu." "Husema (La!) Bali tutafuata tuliowakuta nayo wazee wetu." "Basi watawafuata tu hao wazee wao hata wakiwa katika upotofu ulio dhahiri."

"Basi hao ndio waliokhitari upotofu kuliko uwongofu na wakakhitari adhabu (ya Mwenyezi Mungu) kuliko maghufira yake." Na "Basi labda wanaweza kuvumilia adhabu ya Moto wa Mwenyezi Mungu." "Ilimu ya kufuatwa ni ilimu inayosema Mwenyezi Mungu amesema hivi, Mtume amesema hivi."

Katika hii Aya waliyoifanya ya 8 wanapindua vile vile tamko la *Arsh* kama walivyofanya tukawajibu katika Aya ya 3 ya *Surat Yunus*.

12. Mwenyezi Mungu anazidi kumtia nguvu Mtume asife moyo kwa ajili ya stihzai na kejeli na shere zinazomkuta katika kufundisha dini. Baadhi ya stihzai zao ni kama hivyo kumwambia:– Kama kweli wewe ni Mtume, mbona umasikini? Kwa nini Mungu wako hakuteremshii khazina; Au kwa nini Mungu asimpe Malaika kufuatana naye ili kuwapa habari watu kuwa yeye ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?

13. Makafiri wakimwambia Mtume kuwa hiyo Qurani ameitunga Yeye mwenyewe Mtume, sio Mwenyezi

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوَرٍ مِّثْلِهِ
مُفْتَرَيَاتٍ وَادْعُوا مَنِ اسْتَطَعْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ
إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٣﴾

13. Ndiyo kweli wanasema kuwa: "Amekitunga mwenyewe (Muhammad kitabu hiki)?" Sema: "Basi leteni sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii, na weteni muwawezao (kuweta) badala ya Mwenyezi Mungu (waje wakusaidieni kutunga hivyo) ikiwa mnasema kweli.

فَإِلَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّمَا أُنزِلَ بِعِلْمِ
اللَّهِ وَأَن لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ فَهَلْ أَنتُم مُّسْلِمُونَ ﴿١٤﴾

14. Na kama hawakukuitikieni, basi jueni ya kwamba kimeteremshwa kwa ilimu ya Mwenyezi Mungu, na ya kwamba hakuna Mola ila Yeye tu. Basi je! Mtakuwa wanyenyekevu (sasa)?.

مَن كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ
إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٥﴾

15. Wanaotaka maisha ya dunia na mapambo yake, tutawapa humu duniani (ujira wa) vitendo vyao kamili; humu wao hawatapunjwa (lakini Akhera hawatapata kitu).

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ ۖ
وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبَاطِلٌ مَّا كَانُوا
يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

16. Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu katika Akhera ila Moto, na yataruka tupu waliyoyafanya katika (dunia) hii, na yatakuwa bure waliyokuwa wakiyatenda.

أَفَمَن كَانَ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ
مِّنْهُ وَمِن قَبْلِهِ كِتَابُ مُوسَىٰ إِمَامًا وَرَحْمَةً ۚ
أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۚ وَمَن يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ
فَالنَّارُ مَوْعِدُهُ ۚ فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّنْهُ ۚ إِنَّهُ الْحَقُّ
مِن رَّبِّكَ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٧﴾

17. Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola wake, (Naye ni Nabii Muhammad) na anaifuata (dalili hiyo) shahidi atokaye kwake Mwenyezi Mungu, (Nayo ni Qurani); na kabla yake kilikuwa Kitabu cha Musa kilichokuwa kiongozi na rehema (Nayo ni Taurati ambayo ilitaja habari ya Nabii Muhammad) (anaweza kuwa muongo? Hawezi kuwa muongo. Basi) hao (walioongoka) wanamuamini yeye; na atakayemkataa katika makundi (ya maadui), basi Moto ndio mahali pa miadi yao. Basi usiwe na shaka juu ya hayo. Hii ni haki itokayo kwa Mola wako; lakini watu wengi hawaamini.

---

Mungu ameiteremsha. Basi ndio wanaambiwa hapa kuwa Mkiwa mnasema kuwa maneno hayo yanaweza kutungwa na binadamu — nayo ameyatunga Yeye Nabii Muhammad — basi na nyinyi tungeni walau sura kumi tu.

15. Uitake dunia na Akhera, na Akhera ndiyo zaidi. Sio kutaka dunia tupu. Hapo utaangamia.

17. Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ya 18 wametia ukafiri wao tena wa kumdaia mtu wao Utume na Unabii Isa. Na ukafiri huu tumejibu katika Marejezo ya Aya ya 7 ya *Al Faatiha* na Aya ya 4 na 115 za *Suratul Baqarah*. Waongo kweli kweli waliposema: "Wakati mafundisho ya Kiislamu yamefanyiwa shaka hasa ni baada ya mwaka elfu moja mia tatu na hamsini." Wanajua kwa yakini kuwa Uislamu ulipata msukosuko wa kweli zama za Al Ustadh Al Imam Muhammad Abdoo, wakati wa nguvu za dola ya Kifaransa, wakati Waziri wa Mambo ya Nje wa dola ya Kifaransa — M. Hanouto — alipozialika dola zote za Kizungu zinazowatawalia Waislamu; akazitaka ziwe mkono mmoja ziuuondoshe Uislamu; ati kwa kuwa ndio unaozulia Ustaarabu usende mbele! Wakakhutubu Maprofesa wao wakubwa wakubwa—na wa dola hizo nyingine—kuthubutisha uwongo wao huo. Na mkubwa wa

18. Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo? Hao watahudhurishwa mbele ya Mola wao, na mashahidi (Malaika wao) watasema: "Hao ndio waliomzulia Mola wao uwongo." Sikilizeni! Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۚ أُولَٰئِكَ يُعْرَضُونَ عَلَىٰ رَبِّهِمْ وَيَقُولُ الْأَشْهَادُ هَٰؤُلَاءِ الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ ۚ أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٨﴾

19. Ambao wanazuilia (watu) na njia ya Mwenyezi Mungu na wanataka ipotoke; na wanaikataa Akhera.

الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿١٩﴾

20. Hao hawawezi kuponyoka katika nchi (akawakosa Mwenyezi Mungu asiwapate); wala hawana walinzi baada ya Mwenyezi Mungu. Watazidishiwa adhabu. Hawawezi kusikia wala hawawezi kuona (kwa uchungu uliowashika wa kuichukia haki, kwa hivyo hawataki kuisikia wala kuiona).

أُولَٰئِكَ لَمْ يَكُونُوا مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ۘ يُضَاعَفُ لَهُمُ الْعَذَابُ ۚ مَا كَانُوا يَسْتَطِيعُونَ السَّمْعَ وَمَا كَانُوا يُبْصِرُونَ ﴿٢٠﴾

21. Hao ndio waliyozitia khasarani nafsi zao, na yatawapotea waliyokuwa wakiyazua.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢١﴾

22. Bila shaka hao ndio wenye khasara ya kweli kweli huko Akhera.

لَا جَرَمَ أَنَّهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمُ الْأَخْسَرُونَ ﴿٢٢﴾

23. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kunyenyekea kwa Mola wao; hao ndio watu wa Peponi; humo watakaa milele.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَخْبَتُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٣﴾

24. Hali ya makundi mawili (haya ya Waislamu na Makafiri) ni kama (mtu) mwenye upofu na uziwi. (Ndiye kafiri huyo), na mtu mwenye kuona na kusikia. (Ndiye Islamu huyo). Je, wawili hawa wanaweza kuwa sawa (katika hali zao)? Basi je, hamufikiri?

مَثَلُ الْفَرِيقَيْنِ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصَمِّ وَالْبَصِيرِ وَالسَّمِيعِ ۚ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۚ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٢٤﴾

25. Na sisi tulimpeleka (tulimtuma) Nuhu kwa watu wake, (akawaambia): "Mimi kwenu ni Muonyaji anayebainisha (kila kitu)

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ ﴿٢٥﴾

26. Ya kwamba msimuabudu yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu; hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya siku (kubwa hiyo) inayoumiza."

أَنْ لَا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۖ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ أَلِيمٍ ﴿٢٦﴾

---

Maprofesa hao alikuwa M. Renan. Zikatolewa hutuba hizo katika Parliament kubwa ya France. Akenda Sh. Muhammad Abdo akakhutubu naye; akazinyamazisha hoja zao zote hizo, na akazitungia kitabu kizima alichokiita *Al Islam wan Nasraniyya*. Dola zote hizo zikayaona kweli maneno ya Sh. Muhammad Abdo na wenziwe, si ya Renan na wenziwe. Wao wanasema mashaka yalitokea baada ya 1350. Mashaka gani yaliyotokea katika miaka hiyo, na mtu wao alikuweko wapi wakati huo? Hapana shaka kuwa wakati huo mtu wao alikuwa amekwishakuitema dunia zamani, anairamba Akhera. Basi uwongo maneno yao yote hayo. Kujigamba tu huko kwa uwongo kabisa.

20. Hao wanaomuwasi Mwenyezi Mungu hawakumshinda. Amewapa Mwenyewe uweza wa kufanya mema na kufanya mabaya, awalipe kwa mema yao na kwa mabaya yao; hapana kudhulumiwa.

25-48. Habari za Nabii Nuhu na watu wake. Ndiye Mtume wa mwanzo kukumbana na misukosuko mikubwa kabisa. Alikuwa Iraki.

27. Na hapo wakasema wakubwa wa wale, waliokufuru katika kaumu yake: "Hatukuoni ila ni mtu tu sawa nasi; wala hatukuoni ila wamekufuata wale wanaoonekana dhahiri kuwa ni dhaifu (wanyonge) wetu; (wamekufuata) kwa fikira ya mwanzo tu (bila kukupeleleza vizuri); wala hatukuoneni kuwa mnayo ziada juu yetu; bali tunakuoneni kuwa ni waongo tu."

فَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِهِ مَا نَرَاكَ إِلَّا بَشَرًا مِّثْلَنَا وَمَا نَرَاكَ اتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَاذِلُنَا بَادِيَ الرَّأْيِ وَمَا نَرَىٰ لَكُمْ عَلَيْنَا مِن فَضْلٍ بَلْ نَظُنُّكُمْ كَاذِبِينَ ﴿٢٧﴾

28. (Hapo) Akasema: "Enyi watu wangu! Mnaonaje kama ninayo dalili wazi iliyotoka kwa Mola wangu, na amenipa rehema kutoka kwake (ya Utume), nayo ikakufichikieni; je, tutakulazimisheni kuikubali ijapokuwa mnaichukia?"

قَالَ يَا قَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِن كُنتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَآتَانِي رَحْمَةً مِّنْ عِندِهِ فَعُمِّيَتْ عَلَيْكُمْ أَنُلْزِمُكُمُوهَا وَأَنتُمْ لَهَا كَارِهُونَ ﴿٢٨﴾

29. "Na enyi watu wangu! Mimi sikuombeni mali juu ya (jambo) hili; sina ujira wangu ila kwa Mwenyezi Mungu; na mimi sitawafukuza walioamini (kama mlivyotaka kwangu niwafukuze hao madhaifu ndipo msilimu nyinyi watukufu. Sitafanya hivyo); maana wao watakutana na Mola wao (awalipe kwa mema yao na mabaya). Lakini mimi nakuoneni nyinyi ni watu mnaofanya ujinga. (Mnakataa kuifuata haki kwa kuwa imefuatwa na madhaifu)!

وَيَا قَوْمِ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مَالًا إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّهُم مُّلَاقُو رَبِّهِمْ وَلَٰكِنِّي أَرَاكُمْ قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿٢٩﴾

30. "Na enyi watu wangu! Ni nani atakayenisaidia mbele ya Mwenyezi Mungu ikiwa nitawafukuza? Je, hamufikiri?

وَيَا قَوْمِ مَن يَنصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِن طَرَدتُّهُمْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

31. "Wala sikuambieni kuwa nina khazina za Mwenyezi Mungu; wala kuwa mimi najua mambo ya ghaibu; wala sisemi, 'Mimi ni Malaika;' wala sisemi kwa wale ambao yanawadharau macho yenu kuwa Mwenyezi Mungu hatawapa kheri. Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zao. (Nikisema hivi) hapo bila shaka nitakuwa miongoni mwa madhalimu."

وَلَا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ إِنِّي مَلَكٌ وَلَا أَقُولُ لِلَّذِينَ تَزْدَرِي أَعْيُنُكُمْ لَن يُؤْتِيَهُمُ اللَّهُ خَيْرًا اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا فِي أَنفُسِهِمْ إِنِّي إِذًا لَّمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٣١﴾

32. Wakasema: "Ewe Nuhu! Umejadiliana nasi na umekithirisha (umezidisha) majadiliano nasi, basi tuletee unayotuahidi; (kuwa tutaadhibiwa); ukiwa miongoni mwa wanaosema kweli."

قَالُوا يَا نُوحُ قَدْ جَادَلْتَنَا فَأَكْثَرْتَ جِدَالَنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣٢﴾

---

27. Hii ndiyo ada yao matajiri — kila asiyekuwa tajiri, si mtu kwao wala si kitu — ni mdhalilifu hawezi kupata lolote hata kwa Mungu. Mungu hatazami mali; anatazama nia na amali. Na wanawajua kuwa si waongo. Basi tu, wanawatukana.

31. Mitume, katika Qurani yote nzima na katika maneno yao, wanajikatalia kujua ghaibu (mambo yaliyofichikana) ila waletewe Wahyi wa Mwenyezi Mungu wa kujulishwa jambo hilo. Na kuna watu tele wanaowathubutishia vipenzi vyao sifa hii, na wenyewe wakajikubalia pia, bali na wakajisingizia hayo na wakajigambia. Na Mwenyezi Mungu anayakanusha haya kabisa katika Qurani yote nzima. Basi uwongo, hawayajui yaliyo katika siri ya Mungu; wanadanganya kama wanavyodanganya wachawi. Na mengi katika hayo wanayonasibishwa ni uwongo tu. Hayakutokea chochote. Hakuna awezaye kuleta alitakalo. Tazama hii Aya 33.

33. Akasema: "Mwenyezi Mungu atayaleta kwenu akipenda, na nyinyi hamtaweza kumshinda."

قال إنما يأتيكم به الله إن شاء وما أنتم بمعجزين ﴿٣٣﴾

34. "Wala haitakufaeni nasaha yangu nikitaka kukunasihini, kama Mwenyezi Mungu anataka kukuacheni kupotea. Yeye ndiye Mola wenu; na kwake mtarejeshwa."

ولا ينفعكم نصحي إن أردت أن أنصح لكم إن كان الله يريد أن يغويكم هو ربكم وإليه ترجعون ﴿٣٤﴾

35. Ndiyo kweli wanasema (makafiri wa Makka kuwa Mtume) "Ameitunga (mwenyewe) hii (Qurani)?" Sema: "Kama nimeitunga basi jukumu langu ni juu yangu (mwenyewe, halikukhusuni kitu); na mimi ni mbali na jukumu lenu (kwa mnayoyafanya nyinyi, hayanikhusu kitu vile vile)."

أم يقولون افتراه قل إن افتريته فعلي إجرامي وأنا بريء مما تجرمون ﴿٣٥﴾ ع

36. Na akafunuliwa Nuhu (akaletewa Wahyi) kuwa "Hataamini (sasa) yoyote katika watu wako isipokuwa wale wale waliokwishaamini; kwa hivyo usisikitike kwa yale waliyokuwa wakiyatenda."

وأوحي إلى نوح أنه لن يؤمن من قومك إلا من قد آمن فلا تبتئس بما كانوا يفعلون ﴿٣٦﴾

37. "Na unda jahazi mbele ya macho yetu (yaani katika hifdhi yetu, hawataweza kukudhuru) na (iwe sawa na) amri yetu (Wahyi tuliokuletea). Wala usinisemeze (kuwasamehe) wale waliodhulumu (nafsi zao kwani sitawasamehe), kwa yakini wao watazamishwa."

واصنع الفلك بأعيننا ووحينا ولا تخاطبني في الذين ظلموا إنهم مغرقون ﴿٣٧﴾

38. Na akawa anaunda jahazi; na kila wakimpitia maraisi makafiri wa umma wake walikuwa wakimcheka, na yeye husema: "Kama nyinyi mnatucheka, nasi tutakuchekeni kama mnavyotucheka."

ويصنع الفلك وكلما مر عليه ملأ من قومه سخروا منه قال إن تسخروا منا فإنا نسخر منكم كما تسخرون ﴿٣٨﴾

39. "Karibuni hivi mtajua ni nani itakayemjia adhabu ya kumhizi (kumfedhehesha) na itakayemteremkia adhabu itakayokaa (naye maisha)."

فسوف تعلمون من يأتيه عذاب يخزيه ويحل عليه عذاب مقيم ﴿٣٩﴾

40. Hata ilipokuja amri yetu, na ardhi ikaanza kufoka maji tulimwambia: "Pakia humo (jahazini) jozi moja katika kila (nyama, jike na dume,) na (wapakie) watu wako wa nyumbani kwako isipokuwa wale ambao imewapitia hukumu (ya Mwenyezi Mungu). Na (wachukue wote) walioamini." Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.

حتى إذا جاء أمرنا وفار التنور قلنا احمل فيها من كل زوجين اثنين وأهلك إلا من سبق عليه القول ومن آمن وما آمن معه إلا قليل ﴿٤٠﴾

---

33. Katika hii Aya walıyoifanya ya 34 wanatia uwongo wao — walioutia katika Aya waliyoifanya ni ya 47 ya *Surat Yunus* — wa kusema kuwa Mwenyezi Mungu wakati mwengine haitimu ahadi yake anayoitoa. Tazama jawabu katika marejezo ya hiyo Aya 47 ya *Surat Yunus.*

34. Tumetaja mara nyingi Kwa Aya za Qurani kuwa Mwenyezi Mungu anawaongoa wanaokubali kufuata haki, na anawaachia kupotea wasiotaka wenyewe kuongoka.

41. Na akasema (Nuhu): "Pandeni humo, kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwe kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu."

وَقَالَ ارْكَبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ مَجْرٖىهَا وَمُرْسٰىهَا
إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٤١﴾

42. Ikawa hiyo (jahazi) inakwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamwita mwanawe aliyekuwa mbali (amekataa kuingia jahazini): "Ewe mwanagu! Panda pamoja nasi wala usiwe pamoja na makafiri."

وَهِيَ تَجْرِي بِهِمْ فِي مَوْجٍ كَالْجِبَالِ وَنَادَىٰ نُوحٌ
ابْنَهُ وَكَانَ فِي مَعْزِلٍ يَا بُنَيَّ ارْكَب مَّعَنَا وَلَا
تَكُن مَّعَ الْكَافِرِينَ ﴿٤٢﴾

43. Akasema (huyo mtoto): "Nitaukimbilia mlima utakaonilinda na maji." Akasema (Nuhu): "Hakuna leo wa kulindwa na amri ya Mwenyezi Mungu isipokuwa yule atakayemrehemu (Mwenyezi Mungu)." Mara mawimbi yakaingia baina yao na akawa miongoni mwa waliogharikishwa.

قَالَ سَآوِي إِلَىٰ جَبَلٍ يَعْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ ۚ قَالَ
لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَن رَّحِمَ ۚ وَحَالَ
بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٤٣﴾

44. Na (baada ya kuangamizwa wote na vyote alivyotaka Mwenyezi Mungu viangamie) ikasemwa: "Ewe ardhi! Meza maji yako. Na Ewe mbingu! Jizuie (na kuteremsha mvua)." Basi Maji yakadidimia chini na amri ikapitishwa (ya kuangamizwa makafiri), na (jahazi) likasimama juu ya (jabali linaloitwa) Judi. Na ikasemwa "Wameangamiliziwa mbali watu madhalimu."

وَقِيلَ يَا أَرْضُ ابْلَعِي مَاءَكِ وَيَا سَمَاءُ أَقْلِعِي وَغِيضَ
الْمَاءُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَاسْتَوَتْ عَلَى الْجُودِيِّ ۖ وَقِيلَ
بُعْدًا لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾

45. Na Nuhu alimuomba Mola wake (alipomuona mwanawe anaangamia) akasema: "Ewe Mola wangu! Mwanangu ni katika watu wa nyumbani kwangu (mbona anaangamia)? Na hakika ahadi yako ni haki; nawe ni Mwenye haki kuliko mahakimu (wote)."

وَنَادَىٰ نُوحٌ رَّبَّهُ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ ابْنِي مِنْ أَهْلِي
وَإِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ وَأَنتَ أَحْكَمُ الْحَاكِمِينَ ﴿٤٥﴾

46. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ewe Nuhu! Huyu si miongoni mwa watu wako. Yeye ni (mwenye) mwendo usiokuwa mzuri. Basi usiniombe ambayo huyajui. Mimi nakunasihi usiwe miongoni mwa wajinga."

قَالَ يَا نُوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ ۖ إِنَّهُ عَمَلٌ
غَيْرُ صَالِحٍ ۖ فَلَا تَسْأَلْنِ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۖ
إِنِّي أَعِظُكَ أَن تَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٤٦﴾

---

41. Tamko hili linasomwa kwa E—MAJREHA si MAJRIYHA. Na katika Qiraa cha Imamu Hafsi (ambacho ndicho Qiraa tunachosoma) linasomwa kwa E tamko hili tu. Basi natusome *Majreha* si *Majriyha*. Ukisoma *Majriyha* utapata dhambi. Na hao walimu walowasomesha wanafunzi wao *Majriyha* walikosea; walimu wajuzi wakiwasomesha wanafunzi wao *Majreha*.

46. Basi watu wasideke bure wakasema wao wanatokana na hao na hao; hayawafai kitu hayo. Kimfaacho mtu amali zake — sio nasaba yake. Mumemuona mtoto wa Nabii Nuhu alivyoangamizwa pamoja na wabaya wenziwe. Hakukumsaidia lolote kule kuzaliwa kwake na Nabii Nuhu. Na Mwenyezi Mungu ametubainishia dhahiri shahiri katika Qurani kuwa mabwana wazuri hao katika vizazi vyao walipatikana wabaya (ambao watakuwa Motoni pamoja na wabaya wenzao) na walipatikana wazuri (ambao watakuwa Peponi pamoja na wazuri wenzao kama hao wazee wao). Alisema Mwenyezi Mungu haya katia Aya ya 124 ya *Suratul Baqarah*. Na akasema katika Aya ya 113 ya *Suratus Saffat* na kwengineko. Na Mtume amesema:- 'Yo yote yule ambaye amali zake zitamweka nyuma basi nasaba yake haitampeleka mbele' wala haina utukufu naye wowote nasaba hiyo katika dini. Katika dini Mwenyezi

47. (Nuhu) akasema: "Ee Mola wangu! Mimi najikinga kwako nisije kukuomba (tena) nisiyoyajua; na kama hutanisamehe na kunirehemu, nitakuwa miongoni mwa watakaopata khasara."

قَالَ رَبِّ إِنِّيٓ أَعُوذُ بِكَ أَنْ أَسْـَٔلَكَ مَا لَيْسَ لِي بِهِۦ عِلْمٌ ۖ وَإِلَّا تَغْفِرْ لِي وَتَرْحَمْنِيٓ أَكُن مِّنَ الْخٰسِرِينَ ﴿٤٧﴾

48. Ikasemwa: "Ewe Nuhu! Shuka (katika nchi kavu sasa) kwa salama itokayo kwetu na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe. Na zitakuwako umma (baada yako) tutakazozistarehesha, kisha zitawashika kutoka kwetu adhabu zinazoumiza."

قِيلَ يٰنُوحُ اهْبِطْ بِسَلٰمٍ مِّنَّا وَبَرَكٰتٍ عَلَيْكَ وَعَلٰىٓ أُمَمٍ مِّمَّن مَّعَكَ ۚ وَأُمَمٌ سَنُمَتِّعُهُمْ ثُمَّ يَمَسُّهُم مِّنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٨﴾

49. Hizi ni katika khabari za siri tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Qurani kuteremshwa). Basi subiri; hakika mwisho (mwema) utawathubutikia wanaomcha Mungu.

تِلْكَ مِنْ أَنۢبَآءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَآ إِلَيْكَ ۖ مَا كُنتَ تَعْلَمُهَآ أَنتَ وَلَا قَوْمُكَ مِن قَبْلِ هٰذَا ۖ فَاصْبِرْ ۖ إِنَّ الْعٰقِبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٩﴾

50. Na kwa Kina Adi tuliwapelekea ndugu yao, Hud. Akasema: "Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu; nyinyi hamna Mungu isipokuwa Yeye. Hamkuwa nyinyi ila ni watungao uwongo tu (katika kusema masanamu kuwa washirika wa Mwenyezi Mungu)."

وَإِلٰى عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۚ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلٰهٍ غَيْرُهُۥٓ ۖ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا مُفْتَرُونَ ﴿٥٠﴾

51. "Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira juu ya haya. Haukuwa ujira wangu ila kwa Yule aliyeniumba. Basi hamyatii akilini (haya ninayokwambieni)?"

يٰقَوْمِ لَآ أَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى الَّذِي فَطَرَنِيٓ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾

52. "Na enyi watu wangu! Ombeni msamaha kwa Mola wenu (kwa mabaya yenu yaliyopita), kisha mtubie kwake (kwa kufanya mema sasa na kuacha mabaya), atakuleteeni mawingu yateremshayo mvua tele, na atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu (mlizonazo). Wala msikengeuke kuwa waovu."

وَيٰقَوْمِ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوٓا إِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَآءَ عَلَيْكُم مِّدْرَارًا وَيَزِدْكُمْ قُوَّةً إِلٰى قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِينَ ﴿٥٢﴾

53. Wakasema: "Ewe Hudi! Hujatuletea dalili zilizo wazi (za kuonyesha ukweli wa maneno yako

قَالُوا يٰهُودُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِيٓ

---

Mungu anasema 'Walio bora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale wacha Mungu wenu.' Na Ucha Mungu hauna Certificate, ikawa mtu akishapata shahada hiyo atajihisabu kuwa yeye ashakuwa katika kumbo hilo. Shahada hiyo iko kwa Mungu tu ndiye anayeitoa siku ya Kiama, haiko midomoni mwake mwenyewe huyo mtu wala katika mavazi yake wala katika midomo ya vipenzi vyake na wafuasi wake. Anasema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 32 ya *Suratun Najm;* "Basi msizitakase (msizisifu) nafsi zenu; Yeye anamjua sana aliyetakasika (na asiyetakasika)."

Hata katika sahifa ya 4 ya juzuu ya kwanza ya Hashiya ya Ashsharqawy juu ya Sherehe ya Sheikh Zakariyyal Ansary juu ya kitabu chake alichokiita *Tahriru Tanqyhil Lubab* imeandikwa kuwa Ubora wa mtu katika Uislamu umo katika kusoma ilimu akafuata, haumo katika nasaba yake. Amesema; "Wenye ilimu ni bora kuliko Masharifu wasio kuwa na ilimu."

50-60. Habari za Nabii Hudi na watu wake. Walikuwa kusini ya Bara Arabu. Naye ndiye Mtume wa pili baada ya Nabii Nuhu.

51. Haya ni kama yale tuliyoyasema katika Aya ya 26 ya Sura hii hii.

53. Wanasema uwongo kusudi. Walipewa chungu za hoja na dalili.

آلِهَتِنَا عَن قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٥٣﴾

unayotwambia); wala sisi hatuwezi kuiacha miungu yetu kwa usemi wako; wala sisi hatutakuwa wenye kukuamini wewe."

إِن نَّقُولُ إِلَّا اعْتَرَاكَ بَعْضُ آلِهَتِنَا بِسُوءٍ ۗ
قَالَ إِنِّي أُشْهِدُ اللَّهَ وَاشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا
تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾

54. "Hatusemi ila kuwa baadhi ya miungu yetu imekwishakukutia baani (kwa vile unavyoitukana)." Akasema: "Mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, nanyi shuhudieni, ya kwamba mimi niko mbali na hao mnaowashirikisha (na Mungu)"

مِن دُونِهِ ۖ فَكِيدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونِ ﴿٥٥﴾

55. "Mkamuacha yeye. (Siwaogopi siwabali). Basi nyote nifanyieni hila (za kunidhuru, na kuniua wala) kisha msinipe muhula wo wote."

إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُم ۚ
مَّا مِن دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا ۚ إِنَّ رَبِّي
عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

56. "Mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Hakuna kiumbe yo yote isipokuwa (Mwenyezi Mungu) anamsarifu atakavyo. Bila shaka Mola wangu yuko juu ya njia iliyonyoka."

فَإِن تَوَلَّوْا فَقَدْ أَبْلَغْتُكُم مَّا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ ۚ
وَيَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّونَهُ شَيْئًا ۚ
إِنَّ رَبِّي عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ ﴿٥٧﴾

57. "Na kama mtarudi nyuma (hainidhurishi kitu); nimekwisha kukufikishieni niliyotumwa nayo kwenu; na Mola wangu atawafanya makhalifa (wakazi wa mahali hapa) watu wengine wasiokuwa nyinyi; wala nyinyi hamtaweza kumdhuru hata kidogo. Hakika Mola wangu ni Mwenye kuhifadhi kila kitu."

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا هُودًا وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ
بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَنَجَّيْنَاهُم مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٨﴾

58. Ilipofika amri yetu ya (kuangamizwa) tulimuokoa Hudi na wale walioamini pamoja naye— kwa rehema itokayo kwetu. Na tukawaokoa katika adhabu ngumu.

وَتِلْكَ عَادٌ ۖ جَحَدُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ وَعَصَوْا رُسُلَهُ
وَاتَّبَعُوا أَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٥٩﴾

59. Na hao ndio Adi. Walikanusha Aya za Mola wao, na wakawaasi Mitume Yake, na wakafuata amri ya kila jabari mkaidi.

وَأُتْبِعُوا فِي هَٰذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ
أَلَا إِنَّ عَادًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ ۗ أَلَا بُعْدًا لِّعَادٍ قَوْمِ
هُودٍ ﴿٦٠﴾

60. Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na siku ya Kiama. Sikilizeni. Hakika Adi walimkufuru Mola wao. Wakaangamizwa hao Adi kaumu ya Hudi.

وَإِلَىٰ ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا ۚ قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا

61. Na kwa Thamudu tukampeleka ndugu yao, Saleh. Akasema: "Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu; nyinyi hamna Mungu ila Yeye.

---

54-56. Nabi Hudi anawabainishia kuwa hao wanaowaabudu hawana lao jambo — hawawezi kudhuru wala kunufaisha. Na anawatia mori (challenge) wamdhuru kama wataweza. Na wewe uwachalenji wanaokutishia kwa mizimu yao na mapango yao na makaburi yao na . . . Usiogope.

61-68. Habari za Nabii Saleh na watu wake. Walikuwa kaskazini ya Bara Arabu. Watatu baada ya Nabii Nuhu.

Nguvu zao na za Mola — Bora zipi.
Mambo yote ni ya Mungu — Atakalo ndilo huwa
Ndiye pweke — Mwenye quwa
Mwenye amri — Na shani

Yeye ndiye aliyekuumbeni katika ardhi, na akakukalisheni humo. Basi muombeni msamaha (kwa makosa yenu yaliyopita), kisha mrejee Kwake. Hakika Mola wangu ni karibu (na waja Wake); anapokea (maombi yao).

ٱللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُۥ ۖ هُوَ أَنشَأَكُم مِّنَ
ٱلْأَرْضِ وَٱسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَٱسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ
تُوبُوٓا۟ إِلَيْهِ ۚ إِنَّ رَبِّى قَرِيبٌ مُّجِيبٌ ٦١

62. Wakasema: "Ewe Saleh! Bila shaka ulikuwa unayetarajiwa (kheri) kwetu kabla ya haya. (Sasa umeharibika). Oh! Unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tumo katika shaka inayotusugua (katika nyoyo zetu) kwa haya unayotuitia."

قَالُوا۟ يَٰصَٰلِحُ قَدْ كُنتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَٰذَآ ۖ
أَتَنْهَىٰنَآ أَن نَّعْبُدَ مَا يَعْبُدُ ءَابَآؤُنَا وَإِنَّنَا
لَفِى شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَآ إِلَيْهِ مُرِيبٍ ٦٢

63. Akasema: "Enyi watu wangu! Mnaonaje, kama ninazo dalili zilizo wazi zitokazo kwa Mola wangu (za kunionyesha ukweli wa haya), naye amenipa rehema kutoka kwake, basi ni nani atakayeninusuru kwa Mwenyezi Mungu kama nikimuasi? Basi hamtanizidishia (kwa hayo mnayonitakia) ila khasara.

قَالَ يَٰقَوْمِ أَرَءَيْتُمْ إِن كُنتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن
رَّبِّى وَءَاتَىٰنِى مِنْهُ رَحْمَةً فَمَن يَنصُرُنِى مِنَ
ٱللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُۥ ۖ فَمَا تَزِيدُونَنِى غَيْرَ تَخْسِيرٍ ٦٣

64. Na enyi watu wangu! Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu ni Ishara kwenu (mliyoitaka kwangu ili kuonyesha ukweli wa Utume wangu). Basi muacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu; wala msimguse kwa ubaya isije ikakuangamizeni adhabu iliyo karibu (na kukufikieni)."

وَيَٰقَوْمِ هَٰذِهِۦ نَاقَةُ ٱللَّهِ لَكُمْ ءَايَةً فَذَرُوهَا
تَأْكُلْ فِىٓ أَرْضِ ٱللَّهِ ۖ وَلَا تَمَسُّوهَا بِسُوٓءٍ
فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابٌ قَرِيبٌ ٦٤

65. Wakamchinja. Basi (Saleh) akasema: "Stareheni katika mji wenu huu (muda wa) siku tatu (tu, kisha mtaadhibiwa); hiyo ni ahadi isiyokuwa ya uwongo."

فَعَقَرُوهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوا۟ فِى دَارِكُمْ ثَلَٰثَةَ
أَيَّامٍ ۖ ذَٰلِكَ وَعْدٌ غَيْرُ مَكْذُوبٍ ٦٥

66. Basi ilipofika amri yetu, tukamuokoa Saleh na wale walioamini pamoja naye kwa rehema Yetu; na (pia tukawaokoa) katika hizaya ya siku hiyo. Hakika Mola wako ndiye Mwenye nguvu (na) Mwenye kushinda.

فَلَمَّا جَآءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا صَٰلِحًا وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
مَعَهُۥ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَمِنْ خِزْىِ يَوْمِئِذٍ ۗ
إِنَّ رَبَّكَ هُوَ ٱلْقَوِىُّ ٱلْعَزِيزُ ٦٦

67. Na wale waliodhulumu (nafsi zao) uliwaangamiza ukelele (uliopigwa na Malaika);

وَأَخَذَ ٱلَّذِينَ ظَلَمُوا۟ ٱلصَّيْحَةُ فَأَصْبَحُوا۟ فِى

---

62. Hawana shaka yoyote. Wanajidai tu. Kila shaka wameondoshewa kwa hoja dhahiri.

64. Katika miujiza yao waliyoitaka kwa Nabii Saleh ni kuwa aliambie jabali lipasuke atoke ngamia mwenye mimba pevu, ashikwe na uchungu papo hapo na azae papo hapo mbele yao. Wakafanyiwa haya waliyoyataka. Lakini wakaambiwa tangu siku hiyo wawe wanatumia maji — ya mito na visima na mengineyo — kwa zamu: siku moja wateke wao; siku ya pili ayanywe ngamia, wasiyapate wao hata chembe. Wakenda na haya muda mfupi, kisha wakaona taabu, wakamwua yule ngamia; wakapewa muda wa siku tatu kutubia. Zilipopita siku tatu bila ya kutubia, adhabu iliwajia, wakaangamia.

65. Katika Aya hii wanapinga tena ule muujiza wa yule ngamia, na tumekwisha kuwajibu katika maelezo ya Aya ya 73 ya *Suratula Aaraf*.

66. Hii inasomwa *Yawmiidhin* si *Yawmaidhin*.

دِيَارِهِمْ جٰثِمِيْنَ ﴿٦٧﴾

wakapambazukiwa wametulia tu (wamekufa) katika majumba yao.

كَأَنْ لَّمْ يَغْنَوْا فِيْهَا ۗ اَلَآ اِنَّ ثَمُوْدَاْ كَفَرُوْا
رَبَّهُمْ ۗ اَلَا بُعْدًا لِّثَمُوْدَ ﴿٦٨﴾

68. Kama kwamba hawakuwamo humo. Sikilizeni. Hakika Thamudu walimkufuru Mola wao; basi Thamudu wamepotelea mbali.

وَلَقَدْ جَآءَتْ رُسُلُنَآ اِبْرٰهِيْمَ بِالْبُشْرٰى قَالُوْا
سَلٰمًا ۗ قَالَ سَلٰمٌ فَمَا لَبِثَ اَنْ جَآءَ بِعِجْلٍ حَنِيْذٍ ﴿٦٩﴾

69. Na wajumbe wetu (Malaika kwa sura za kibinadamu) walimwendea Ibrahimu kwa bishara (khabari njema kuwa atazaa na kujukuu na mengine na) wakasema: "Salam (alaykum — amani juu yenu)" Akasema (Ibrahimu) "Juu yenu pia iwe amani." Na hakukaa (Ibrahimu) ila mara alileta ndama (aliyechomwa vizuri juu ya mawe ya moto).

فَلَمَّا رَآٰ اَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ اِلَيْهِ نَكِرَهُمْ وَاَوْجَسَ
مِنْهُمْ خِيْفَةً ۗ قَالُوْا لَا تَخَفْ اِنَّآ اُرْسِلْنَآ اِلٰى
قَوْمِ لُوْطٍ ﴿٧٠﴾

70. Basi alipoona (Ibrahimu) mikono ya (watu) wale haikifikilii (chakula kile) aliwatilia shaka na akawaogopa (akadhani kuwa ni maadui). Wakasema: "Usiogope, hakika sisi tunapelekwa kwa watu wa Luti (tukawaangamize na tukupe khabari wewe na mkeo, Sara, kuwa mtazaa na kujukuu na bado muhai)."

وَامْرَاَتُهٗ قَآئِمَةٌ فَضَحِكَتْ فَبَشَّرْنٰهَا بِاِسْحٰقَ ۙ
وَمِنْ وَّرَآءِ اِسْحٰقَ يَعْقُوْبَ ﴿٧١﴾

71. Na mkewe (Ibrahimu—Bibi Sara) alikuwa kasimama wima (anawatumika); akacheka (aliposikia hivyo). Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haqa na baada ya Is-haq (watapata mjukuu wamwite) Yaakubu.

قَالَتْ يٰوَيْلَتٰٓى ءَاَلِدُ وَاَنَا عَجُوْزٌ وَّهٰذَا بَعْلِيْ
شَيْخًا ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجِيْبٌ ﴿٧٢﴾

72. (Mkewe Ibrahimu) akasema: "Ee Mimi we! Nitazaa na hali mimi ni mkongwe, na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu."

قَالُوْٓا اَتَعْجَبِيْنَ مِنْ اَمْرِ اللّٰهِ رَحْمَتُ اللّٰهِ وَبَرَكٰتُهٗ
عَلَيْكُمْ اَهْلَ الْبَيْتِ ۗ اِنَّهٗ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ ﴿٧٣﴾

73. Wakasema (wale Malaika): "Je, Unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye anayestahiki kusifiwa na kutukuzwa."

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ اِبْرٰهِيْمَ الرَّوْعُ وَجَآءَتْهُ
الْبُشْرٰى يُجَادِلُنَا فِيْ قَوْمِ لُوْطٍ ﴿٧٤﴾

74. Basi khofu ilipomwondokea Ibrahimu na ikawa imemjia ile khabari njema, alianza kubishana nasi (kushindana na Malaika wetu) juu ya watu wa Luti (kuwaombea wasiangamizwe).

اِنَّ اِبْرٰهِيْمَ لَحَلِيْمٌ اَوَّاهٌ مُّنِيْبٌ ﴿٧٥﴾

75. Kwa yakini Ibrahimu alikuwa mpole, mwenye kumtukuza Mwenyezi Mungu na mwepesi wa kurejea (Kwake).

---

69-76. Habari za Nabii Ibrahimu Mtume wane mashuhuri baada ya Nabii Nuhu; alikuwa Iraqi, Shamu. Falastini, Misri, Hijazi na kwengine. Alikuwa Mtume mkubwa kabisa. Baada ya Nabii Muhammad (s.a.w.) yeye ndiye wa pili.

76. (Tukamwambia) "Ewe Ibrahimu! Wacha haya. Kwa hakika amri ya Mola wako imekwishakuja (ya kuangamizwa hao watu wa Luti); na hakika hao itawafika adhabu isiyorudishwa."

يَٰٓإِبۡرَٰهِيمُ أَعۡرِضۡ عَنۡ هَٰذَآۖ إِنَّهُۥ قَدۡ جَآءَ أَمۡرُ
رَبِّكَۖ وَإِنَّهُمۡ ءَاتِيهِمۡ عَذَابٌ غَيۡرُ مَرۡدُودٖ ٧٦

77. Na wajumbe wetu waliopomjia (Nabii) Luti alihuzunika kwa ajili yao (hao wageni kwa kuona kuwa watataabishwa wageni hawa. Hakujua kuwa ni Malaika) na akaona taabu kwa ajili yao, na akasema: "Hii ni siku ngumu (kabisa)."

وَلَمَّا جَآءَتۡ رُسُلُنَا لُوطٗا سِيٓءَ بِهِمۡ وَضَاقَ
بِهِمۡ ذَرۡعٗا وَقَالَ هَٰذَا يَوۡمٌ عَصِيبٞ ٧٧

78. Wakafika kaumu yake wakamjia mbio (nyumbani kwake ili wawafanye machafu wale wageni). Na kabla ya haya walikuwa (daima) wakifanya maovu, akasema (Luti) "Enyi kaumu yangu! Hao binti zangu (binti za 'umma wangu walioolewa katika nyumba zenu) ndio wametakasika kwenu (kuwaingilia si wanaume wenzenu). Basi mcheni Mwenyezi Mungu wala msinifedheheshe mbele ya wageni wangu. Je, miongoni mwenu hakuna mtu muongofu (hata mmoja)?"

وَجَآءَهُۥ قَوۡمُهُۥ يُهۡرَعُونَ إِلَيۡهِ وَمِن قَبۡلُ كَانُواْ
يَعۡمَلُونَ ٱلسَّيِّـَٔاتِۚ قَالَ يَٰقَوۡمِ هَٰٓؤُلَآءِ بَنَاتِي
هُنَّ أَطۡهَرُ لَكُمۡۖ فَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَلَا تُخۡزُونِ فِي
ضَيۡفِيٓۖ أَلَيۡسَ مِنكُمۡ رَجُلٞ رَّشِيدٞ ٧٨

79. Wakasema: "Bila shaka umekwishajua haki tulizonazo juu ya binti zako, (lakini hatuzitaki), na unayajua tunayoyataka."

قَالُواْ لَقَدۡ عَلِمۡتَ مَا لَنَا فِي بَنَاتِكَ مِنۡ حَقّٖ
وَإِنَّكَ لَتَعۡلَمُ مَا نُرِيدُ ٧٩

80. Akasema: "Laiti ningalikuwa na nguvu kwenu (mimi mwenyewe) au nategemea katika nguzo yenye nguvu (watu wenye nguvu ili wanisaidie juu yenu)."

قَالَ لَوۡ أَنَّ لِي بِكُمۡ قُوَّةً أَوۡ ءَاوِيٓ إِلَىٰ رُكۡنٖ
شَدِيدٖ ٨٠

81. (Wale wajumbe) wakasema: "Ewe Luti! Sisi ni wajumbe wa Mola wako (Malaika). Hawatakufikia (kwa baya lolote). Na ondoka pamoja na watu wako katika sehemu ya pingapinga la usiku. Wala yoyote miongoni mwenu asitazame nyuma

قَالُواْ يَٰلُوطُ إِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَن يَصِلُوٓاْ
إِلَيۡكَۖ فَأَسۡرِ بِأَهۡلِكَ بِقِطۡعٖ مِّنَ ٱلَّيۡلِ

---

71. Mwanamke kudhihiri mbele ya wanaume kwa sitara — haonekana ila uso tu na vitanga vya mikono — haikatazwi.

77-83. Huyu ni Mtume wa tano baada ya Nabii Nuhu. Ni mtoto wa ndugu yake Nabii Ibrahimu na mfuasi wake kila mahala alipokwenda. Na mwisho wake akapewa naye Utume . . .

Akawendea hao watu waliokuwa wakifanya maasi ya wanaume wenyewe kwa wenyewe waliokuwa wakikaa hii sehemu iliyo Falastini sasa na iliyo Ardun (Jordan) na kwenye hili ziwa la Dead Sea. Akapata tabu kubwa kabisa kwao kwa ajili ya maasi yao hayo na mengineyo mengi yaliyo mabaya vile vile.

Katika maasi yaliyokhusiana na tupu (a) Mwanamume na mwanamke (b) wanawake wenyewe kwa wenyewe (c) Wanaume kwa wanaume — hili la wanaume kwa wanaume lina taathira mbaya zaidi, kwa hivyo uma huo uliadhibiwa kwa adhabu kubwa zaidi kuliko uma wowote ule kwa madhambi yake yoyote yale.

Na kwa miaka mingi sana madhambi haya yamepiga Goma katika uma wetu huu; na tunayaona haya yanayowapata.

79. Wanayapindua makadiyani maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 80. Hatujui wana itifaki gani na wabaya hao wa Qawmu Lut, hata wakawapigania hivyo. Siri yao wanaijuiwa wenyewe.

وَلَا يَلْتَفِتْ مِنكُمْ أَحَدٌ إِلَّا امْرَأَتَكَ ۖ إِنَّهُ مُصِيبُهَا
مَا أَصَابَهُمْ ۚ إِنَّ مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ ۚ أَلَيْسَ الصُّبْحُ
بِقَرِيبٍ ﴿٨١﴾

(ataposikia vishindo vya kuangamizwa hao wabaya asije akarukwa na akili kwa kuona adhabu kali hiyo). Isipokuwa mke wako (mwanamke mbaya huyo hatakufuata). Naye utampata msiba utakaowapata hao. Hakika miadi yao ni asubuhi. Jee, asubuhi si karibu tu? (Basi tuliza moyo wako. Umekwishafika wakati wao wa kuangamizwa)."

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا جَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا
عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ مَّنضُودٍ ﴿٨٢﴾

82. Basi ilipofika amri yetu, tuliifanya (ardhi hiyo iwe juu chini); juu yake kuwa chini yake, na tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu (wa Motoni uliyokamatana

مُّسَوَّمَةً عِندَ رَبِّكَ ۖ وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ
بِبَعِيدٍ ﴿٨٣﴾

83. (Changarawe) zilizotiwa alama kwa Mola wako (kila moja kuwa ya mtu fulani). Na (adhabu) hii haiko mbali na madhalimu (wengine kama hawa watu wa umma huu wanaofanya machafu haya).

وَإِلَىٰ مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۚ قَالَ يَا قَوْمِ
اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ ۖ وَلَا
تَنقُصُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ ۚ إِنِّي أَرَاكُم بِخَيْرٍ وَإِنِّي
أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ مُّحِيطٍ ﴿٨٤﴾

84. Na kwa watu wa Madyan (tulimpeleka) ndugu yao, Shuebu. Akasema: "Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Msipunguze kipimo (cha vibaba) wala (cha) mizani. Mimi nakuoneni mumo katika hali njema (basi msiiharibu kwa kufanya dhulma). Nami nakukhofieni adhabu ya siku (kubwa) hiyo itakayokuzungukeni."

وَيَا قَوْمِ أَوْفُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۖ وَلَا
تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ
مُفْسِدِينَ ﴿٨٥﴾

85. "Na enyi watu wangu! Timizeni kipimo na mizani kwa uadilifu wala msiwapunguzie watu vitu vyao; wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu."

بَقِيَّتُ اللَّهِ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ۚ
وَمَا أَنَا عَلَيْكُم بِحَفِيظٍ ﴿٨٦﴾

86. "(Mali) aliyokubakishieni Mwenyezi Mungu (kwa njia ya halali) ndiyo bora kwa ajili yenu, ikiwa nyinyi mnaamini. Wala mimi siye mlinzi wenu."

قَالُوا يَا شُعَيْبُ أَصَلَاتُكَ تَأْمُرُكَ أَن نَّتْرُكَ مَا يَعْبُدُ
آبَاؤُنَا أَوْ أَن نَّفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا نَشَاءُ ۖ إِنَّكَ
لَأَنتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ ﴿٨٧﴾

87. Wakasema: "Ewe Shuebu! Sala zako (zinakuzuzua sana)! Zinakuamrisha (utuamrishe) tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Bila shaka wewe ni mwenye akili na mwongofu." (Wanamsifu hivi kwa stihzai na kejeli, siyo kwa hakika).

قَالَ يَا قَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِن كُنتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي
وَرَزَقَنِي مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا ۚ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ

88. Akasema: "Enyi watu wangu! Mnaonaje kama ninayo dalili inayotokana na Mola wangu na ameniruzuku riziki njema (ya Utume) kutoka kwake (nitaacha haya, nishike upotofu wenu)? Wala sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni.

---

80. Anasikitika kuwa yuko peke yake katika hizo nchi za ugeni. Kwao khasa kulikuwa Iraq. Lakini nguzo kubwa anayo — Mwenyezi Mungu. Lakini unyonge wa kibinaadamu ulimgubika.

84-95. Anatajwa Nabii Shuebu na watu wake. Walikuwa katika hizi nchi za Lubnani (Lebanon) na Shamu.

إِلَىٰ مَا أَنْهَاكُمْ عَنْهُ ۚ إِنْ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ مَا
اسْتَطَعْتُ ۚ وَمَا تَوْفِيقِي إِلَّا بِاللَّهِ ۚ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ
وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿٨٨﴾

Sitaki ila kutengeneza, kiasi ninavyoweza. Na sipati kuwezeshwa haya ila na Mwenyezi Mungu (Mwenyewe). Kwake ninategemea, na Kwake naelekea."

وَيَا قَوْمِ لَا يَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِي أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ
مَا أَصَابَ قَوْمَ نُوحٍ أَوْ قَوْمَ هُودٍ أَوْ قَوْمَ صَالِحٍ ۚ
وَمَا قَوْمُ لُوطٍ مِنْكُمْ بِبَعِيدٍ ﴿٨٩﴾

89. "Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni yakakusibuni kama yaliyowasibu watu wa Nuhu au watu wa Hudi au watu wa Salehe. Na watu wa Luti si mbali nanyi." (Karibuni hivi wameangamizwa; na nchi zao ziko karibu na nyinyi pia).

وَاسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ ۚ إِنَّ رَبِّي رَحِيمٌ
وَدُودٌ ﴿٩٠﴾

90. "Na ombeni msamaha kwa Mola wenu (kwa yaliyopita), kisha tubuni kwake (sasa kwa kufanya mema). Hakika Mola wangu ni Mwenye kurehemu na Mwenye kuwapenda (waja Wake)."

قَالُوا يَا شُعَيْبُ مَا نَفْقَهُ كَثِيرًا مِمَّا تَقُولُ وَإِنَّا
لَنَرَاكَ فِينَا ضَعِيفًا ۖ وَلَوْلَا رَهْطُكَ لَرَجَمْنَاكَ ۖ
وَمَا أَنْتَ عَلَيْنَا بِعَزِيزٍ ﴿٩١﴾

91. Wakasema: "Ewe Shuebu! Hatufahamu mengi katika hayo unayoyasema. Na sisi tunakuona mdhalilifu kwetu. Lau kuwa si jamaa zako tungekupiga mawe, wala wewe si mtu mtukufu kwetu! (ila tunachunga hishima ya jamaa zako tu)."

قَالَ يَا قَوْمِ أَرَهْطِي أَعَزُّ عَلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ
وَاتَّخَذْتُمُوهُ وَرَاءَكُمْ ظِهْرِيًّا ۖ إِنَّ رَبِّي بِمَا
تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٩٢﴾

92. Akasema: "Enyi watu wangu! Watu wangu ni watukufu zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu? (Mimi hamnipi hishima kidogo kwa kuwa Mjumbe wa Mungu ila mnanipa kwa ajili ya jamaa zangu!) Na mumemfanya Yeye (Mwenyezi Mungu) yuko nyuma ya migongo yenu. Hakika Mola wangu anayazunguka (kwa kuyajua yote) mnayoyatenda."

وَيَا قَوْمِ اعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ ۖ سَوْفَ
تَعْلَمُونَ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَمَنْ
هُوَ كَاذِبٌ ۖ وَارْتَقِبُوا إِنِّي مَعَكُمْ رَقِيبٌ ﴿٩٣﴾

93. "Na enyi watu wangu! Fanyeni (mtakayo) kwa tamkini yenu; (mtakavyo); na mimi pia ninafanya (yangu kwa tamkini yangu). Karibuni hivi mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ifedheheshayo na ni nani aliye muongo. Na ngojeeni; mimi pia ninangoja pamoja nanyi."

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا شُعَيْبًا وَالَّذِينَ آمَنُوا
مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا
الصَّيْحَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَارِهِمْ جَاثِمِينَ ﴿٩٤﴾

94. Na ilipokuja amri yetu, tulimuokoa Shuebu na wale walioamini pamoja naye kwa rehema yetu. Na wale waliodhulumu ukelele (wa adhabu) ulinyakuwa roho zao. Wakawa majumbani mwao wametulia tu (wamekufa)

كَأَنْ لَمْ يَغْنَوْا فِيهَا ۗ أَلَا بُعْدًا لِمَدْيَنَ كَمَا بَعِدَتْ
ثَمُودُ ﴿٩٥﴾ ع

95. Kama kwamba hawakuwamo humo. Sikilizeni. Wameangamia (watu wa) Madyana kama walivyoangamia (kina) Thamudu.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطَانٍ مُبِينٍ ﴿٩٦﴾

96. Na hakika tulimpeleka Musa pamoja na Aya zetu na hoja zilizo wazi

---

Walikuwa watu wa biashara kubwa kubwa za kwenda mbali kabisa kama tunavyosikia hizo biashara za Phoenicians.

91. Wanafahamu vyema wanavyoambiwa lakini wanajitia pambani kusudi. Asilolitaka mtu hujitia uziwi nalo.

96-99. Miaka mingi kabisa imepita baina ya Nabii Shuebu na Nabii Musa; kwa hivyo si kauli yenye nguvu

97. Kwa Firauni na wakuu (wa umma) wake. Lakini wao walifuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa yenye uongofu.

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَإِيْهِ فَاتَّبَعُوٓا أَمْرَ فِرْعَوْنَ ۖ وَمَآ أَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيدٍ ﴿٩٧﴾

98. Siku ya Kiama (Firauni) atawatangulia watu wake na atawafikisha Motoni. Na ni pabaya palioje mahali hapo panapofikiwa (na maasi wa Mwenyezi Mungu).

يَقْدُمُ قَوْمَهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ فَأَوْرَدَهُمُ ٱلنَّارَ ۖ وَبِئْسَ ٱلْوِرْدُ ٱلْمَوْرُودُ ﴿٩٨﴾

99. Nao wamefuatishiwa laana katika (dunia) hii na siku ya Kiama (pia). Ni mbaya ilioje zawadi watakayopewa hiyo mara mbili (laana ya duniani na laana ya Akhera).

وَأُتْبِعُوا۟ فِى هَٰذِهِۦ لَعْنَةً وَيَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ ۚ بِئْسَ ٱلرِّفْدُ ٱلْمَرْفُودُ ﴿٩٩﴾

100. Hizi ni katika habari za nchi, tunakusimulia. Baadhi yake zipo; na (nyengine) zimefutwa (hazipo tena).

ذَٰلِكَ مِنْ أَنۢبَآءِ ٱلْقُرَىٰ نَقُصُّهُۥ عَلَيْكَ ۖ مِنْهَا قَآئِمٌ وَحَصِيدٌ ﴿١٠٠﴾

101. Nasi hatukuwadhulumu, lakini wao wamejidhulumu wenyewe. Na waungu wao waliokuwa wakiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakuwafaa kitu ilipokuja amri ya Mola wako. Na hao (waungu wao) hawakuwazidishia ila angamizo (tu).

وَمَا ظَلَمْنَٰهُمْ وَلَٰكِن ظَلَمُوٓا۟ أَنفُسَهُمْ ۖ فَمَآ أَغْنَتْ عَنْهُمْ ءَالِهَتُهُمُ ٱلَّتِى يَدْعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ مِن شَىْءٍ لَّمَّا جَآءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَمَا زَادُوهُمْ غَيْرَ تَتْبِيبٍ ﴿١٠١﴾

102. Na namna hivi ndivyo inavyokuwa kutesa kwa Mola wako anapowatesa (watu wa) miji wanapokuwa wameacha mwendo walioambiwa. Hakika teso lake (Mwenyezi Mungu) linaumiza (na) kali kabisa.

وَكَذَٰلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَآ أَخَذَ ٱلْقُرَىٰ وَهِىَ ظَٰلِمَةٌ ۚ إِنَّ أَخْذَهُۥٓ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

103. Kwa yakini katika haya kuna mazingatio kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo siku itakayoshuhudiwa (na viumbe wote).

إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَةً لِّمَنْ خَافَ عَذَابَ ٱلْءَاخِرَةِ ۚ ذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ ٱلنَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ ﴿١٠٣﴾

104. Na hatuiakhirishi ila kwa muda unaohisabiwa (na Mwenyewe Mwenyezi Mungu; utakuja tu).

وَمَا نُؤَخِّرُهُۥٓ إِلَّا لِأَجَلٍ مَّعْدُودٍ ﴿١٠٤﴾

105. Wakati itakapokuja (siku hiyo) kiumbe chochote hakitasema ila kwa ruhusa Yake (Mwenyezi Mungu); basi baadhi yao watakuwa wenye hali mbaya (Nao ni wale maasi) na (wengine) wenye hali nzuri. (Nao ni wale wema).

يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلَّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِۦ ۚ فَمِنْهُمْ شَقِىٌّ وَسَعِيدٌ ﴿١٠٥﴾

106. Ama wale wenye hali mbaya (kwa sababu ya kufanya kwao mabaya), wao watakuwa Motoni, humo wawe wanapiga makelele (ya kama milio ya punda) na kutoa kwikwi

فَأَمَّا ٱلَّذِينَ شَقُوا۟ فَفِى ٱلنَّارِ لَهُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَشَهِيقٌ ﴿١٠٦﴾

---

ile inayosemwa kuwa huyo ndiye aliyekutana naye Madyana.

102. Huwapa muda mrefu kabisa wazingatie, wakitojali baada ya hapo ndipo anapowaangamiza.

107. Watakaa humo milele muda wa kudumu mbingu (za huko) na ardhi (ya huko), isipokuwa apendavyo Mola wako. Hakika Mola wako hufanya apendavyo.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمٰوٰتُ وَالْاَرْضُ اِلَّا مَا شَآءَ رَبُّكَ ۭ اِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيْدُ ﴿١٠٧﴾

108. Na ama wale wenye hali njema (kwa ajili ya wema wao), watakuwa peponi; watakaa humo milele muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipokuwa apendavyo Mola wako. Ni atiya (zawadi) isiyokwisha.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ سُعِدُوْا فَفِي الْجَنَّةِ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمٰوٰتُ وَالْاَرْضُ اِلَّا مَا شَآءَ رَبُّكَ ۭ عَطَآءً غَيْرَ مَجْذُوْذٍ ﴿١٠٨﴾

109. Basi usiwe na shaka juu ya wanayoyaabudu hao (kuwa si waungu hao). Hawaabudu ila kama walivyoabudu wazee wao zamani. Na bila shaka Sisi tutawapa sehemu yao (ya adhabu) kamili bila ya kupunguzwa.

فَلَا تَكُ فِيْ مِرْيَةٍ مِّمَّا يَعْبُدُ هٰٓؤُلَآءِ ۭ مَا يَعْبُدُوْنَ اِلَّا كَمَا يَعْبُدُ اٰبَاۗؤُهُمْ مِّنْ قَبْلُ ۭ وَاِنَّا لَمُوَفُّوْهُمْ نَصِيْبَهُمْ غَيْرَ مَنْقُوْصٍ ﴿١٠٩﴾

110. Na kwa yakini tulimpa Musa Kitabu; (lakini) zikatiwa khitilafu ndani yake (na hao wafuasi wake kwa uzushi wao). Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako (kuwa hawaangamizi sasa), bila shaka ingalihukumiwa baina yao. Na hakika wao wamo katika shaka juu yake inayowahangaisha (inayowakereketa kwa kuona itafuatwa hii dini ya Kiislamu, itangaye).

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ فَاخْتُلِفَ فِيْهِ ۭ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۭ وَاِنَّهُمْ لَفِيْ شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيْبٍ ﴿١١٠﴾

111. Na hakika Mola wako atawapa hao wote malipo ya vitendo vyao sawa sawa. Bila shaka Yeye anazo khabari za (yote) wanayoyatenda.

وَاِنَّ كُلًّا لَّمَّا لَيُوَفِّيَنَّهُمْ رَبُّكَ اَعْمَالَهُمْ ۭ اِنَّهٗ بِمَا يَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿١١١﴾

112. Basi (ewe Mtume)! Endelea na uwongofu kama ulivyoamrishwa; (wewe) na wale wanaoelekea (kwa Mungu) pamoja nawe; wala msiruke mipaka. Hakika yeye anayaona yote mnayoyatenda.

فَاسْتَقِمْ كَمَآ اُمِرْتَ وَمَنْ تَابَ مَعَكَ وَلَا تَطْغَوْا ۭ اِنَّهٗ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿١١٢﴾

---

107. Hapa katika tamko hili "Isipokuwa apendavyo Mola wako. Hakika Mola wako hufanya apendavyo" ndipo walipochukua Stishhadi ulamaa wengine (wasiokuwa Sunni na Shia na Ibadhi) kuwa hata makafiri mwisho wake watasamehewa watolewe Motoni watiwe Peponi.

Ama kwa Kisunni maasi tu (si makafiri) ndio mwisho wao watasamehewa watolewe Motoni watiwe Peponi.

108. Hiyo kauli waliyoitaja katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 109 siyo kauli inayofuatwa na Suni wala Muutazila wala Ibadhi wala Shia. Hiyo ni kauli inayoambiwa kuwa imesemwa na baadhi chache kabisa ya Masahaba na baadhi chache ya Matabiina. Na imesemwa katika Hashiyatul Jamal juu ya Jalaleni kuwa kauli hii kaitia nguvu Imam Ibn Taymiyya na Imam Ibnul Qayyim na wengineo. Wala hakuna kabisa katika *Sahihul Bukhary* kuwa makafiri watatoka Motoni baadaye. Waongo kabisa. Hamuna humo maneno hayo. Wanasema uwongo tu basi. Hapana Aya inayofahamisha kidogo hivi illa hii na aya 128 ya Suratul An-am. Na katika Qurani ndiyo vivyo hivyo. Wanasema uwongo walivyosema: "Katika Qurani mna Aya zinazoonyesha wazi ya kuwa Jahanamu ni kitu cha kupita . . ."

Na katika hii habari ya watu wa Peponi ilipoambiwa "Ni atiya (zawadi) isiyokwisha" imefahamika kuwa Pepo ni ya UMILELE: wala Umilele huo hauchoshi. Eee Umilele wa hapa — usiokuwa na raha tupu—nao hauchoshi, seuze huo usiokuwa na la kuudhi hata moja ila ya kupendwa tu, na kila siku mengine mengine, na kila moja linamshinda mwenziwe kwa uzuri na kupendeza na kushawikisha.

112. Hapana jambo kubwa zaidi kama kutengenea kama alivyosema Mwenyezi Mungu — itatengenea dunia

وَلَا تَرْكَنُوٓا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ
وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَآءَ ثُمَّ لَا
تُنصَرُونَ ﴿١١٣﴾

113. Wala msiwategemee (mkawa pamoja nao) wale wanaodhulumu (nafsi zao kwa maasi); usije ukakuguseni Moto. Na hamtakuwa na mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu; kisha nyinyi hamtasaidiwa (na yoyote huko).

وَأَقِمِ الصَّلَوٰةَ طَرَفَيِ النَّهَارِ وَزُلَفًا مِّنَ الَّيْلِ ۚ
إِنَّ الْحَسَنَٰتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّـَٔاتِ ۚ ذَٰلِكَ ذِكْرَىٰ
لِلذَّٰكِرِينَ ﴿١١٤﴾

114. Na simamisha Sala katika ncha mbili za mchana (nayo ni Adhuhuri na Laasiri) na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. (Nayo ni Magharibi na Isha—ziko karibu na mwisho wa mchana; na Alifajiri iko karibu na mwanzo wa mchana). Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanaokumbuka. (Haya ni mawaidha kwa wanaokubali kuwaidhika).

وَاصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٥﴾

115. Na subiri, kwani Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanaofanya mema.

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْقُرُونِ مِن قَبْلِكُمْ أُولُوا
بَقِيَّةٍ يَنْهَوْنَ عَنِ الْفَسَادِ فِي الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا
مِّمَّنْ أَنجَيْنَا مِنْهُمْ ۗ وَاتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَآ أُتْرِفُوا
فِيهِ وَكَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿١١٦﴾

116. Basi mbona hawakuwamo katika watu wa mbele kabla yenu watu wenye (mabaki ya) akili, wenye kukataza uharibifu katika nchi? Isipokuwa wachache tu miongoni mwao ambao ndio tuliowaokoa. Na wale waliodhulumu (nafsi zao) walifuata waliyostareheshewa. (Nayo ni maasi), na wakawa waovu.

وَمَا كَانَ رَبُّكَ لِيُهْلِكَ الْقُرَىٰ بِظُلْمٍ وَ
أَهْلُهَا مُصْلِحُونَ ﴿١١٧﴾

117. Na Mola wako si wa kuziangamiza nchi kwa dhuluma tu na hali watu wake ni watenda mema. (Hafanyi hivi Mwenyezi Mungu).

وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۖ وَلَا
يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾

118. Na kama Mola wako angalipenda, angaliwafanya watu wote kuwa umati mmoja. (Angaliwafanya wote kufuata kitu kimoja. Lakini amewapa akili na nguvu ya kutumia akili zao hizo watakavyo, ikiwa kwa wema au kwa ubaya). Kwa hivyo wataendelea tu kuhitalifiana

إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ ۚ وَلِذَٰلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ

119. Isipokuwa wale ambao Mola wako amewarehemu; na kwa (rehema) hiyo Mungu amewaumba (ila wenyewe tu hao wengine

---

na Akhera. Amri hii tunapewa siye. Mwenyewe Mtume katengenea sawa sawa.

113. Tumetaja kwa urefu katika Aya ya 85 ya *Suratun Nisaa* wema wa kusaidia kufanyika mema na ubaya wa kusaidia kufanyika mabaya.

114. Kwa huku kusali Sala tano daima Mwenyezi Mungu atamfutia mtu baadhi ya dhambi zake nyingi zilizo baina yake yeye na Mwenyezi Mungu. Na tujitahidi kusali kama tulivyoamrishwa na kufanya mengine yote vile vile kama tulivyoamrishwa na tujiepushe na hayo mabaya pia — makubwa na madogo.

116. Wanalaumiwa sana sana wanavyuoni walioacha kuamrisha mema na kukataza mabaya. Na inaonyesha kuwa hawakupata salama; bali waliangamizwa wanavyuoni hao kama waliovyoangamizwa hao waliokuwa wakiyafanya mabaya hayo, kwani yote haya ni mabaya. Na jaza ya mabaya ni kupata mabaya.

118-119. Mwenyezi Mungu amemuumba binaadamau ili amfanyie mtihani — amtie Peponi akipasi (akifuzu), na amtie Motoni akifeli; kwa hivi akampa utambuzi wa kujua Baya na kujua Jema, na akampa uweza (power) wa kuchagua kufanya atakalo. Hakutiwa masilisili ya kufanya mabaya wala minyororo ya kufanya mema; ili alipwe natija ya mtihani wake kwa haki.

wamekhitari mabaya). Na litatimia neno la Mola wako (la kuwa): "Kweli kweli nitaijaza Jahanamu kwa majini na binaadamu wote (walio wabaya)."

كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾

120. Na tunakusimulia zote katika khabari za Mitume ambazo kwa hizo tunauthubutisha moyo wako. Na katika haya imekujia haki na mauidha na ukumbusho kwa wale wanaoamini.

وَكُلًّا نَّقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنبَاءِ الرُّسُلِ مَا نُثَبِّتُ بِهِ فُؤَادَكَ ۚ وَجَاءَكَ فِي هَٰذِهِ الْحَقُّ وَمَوْعِظَةٌ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٠﴾

121. Na waambie wale wasioamini: "Fanyeni (muyatakayo) kwa tamkini yenu, nasi pia tunafanya (tutakavyo kwa tamkini yetu. Hakuna anayelazimishwa kufuata Uislamu kwa nguvu)

وَقُل لِّلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ اعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنَّا عَامِلُونَ ﴿١٢١﴾

122. Na ngojeni, na sisi tunangojea."

وَانتَظِرُوا إِنَّا مُنتَظِرُونَ ﴿١٢٢﴾

123. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyofichikana katika ardhi na mbingu (na vilivyo dhahiri); na mambo yote yatarejezwa kwake. Basi muabudu yeye na kumtegemea. Na Mola wako haghafiliki na yale mnayoyatenda.

وَلِلَّهِ غَيْبُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَيْهِ يُرْجَعُ الْأَمْرُ كُلُّهُ فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ۚ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٢٣﴾

---

Miongoni mwa Aya hizo zinazoonyesha haya ni Aya 7, 8, 9 na 10 za *Suratush Shams* na Aya ya 12 ya *Suratul Layl* na Aya ya 2 na ya 3 za *Suratud Dahr*, na kama hizo nyingi.

120. Kusikia yaliyowapata wengine na natija nzuri iliyopatikana kunashajiisha moyo, ndiyo maana Mwenyezi Mungu akakithirisha kutaja visa vya wema na vya wabaya, tusione kuwa sisi tumeonewa.

اٰيَاتُهَا ١١١ (١٢) سُوْرَةُ يُوْسُفَ مَكِّيَّةٌ (٥٣) رُكُوْعَاتُهَا ١٢

*Ina Aya 111* **SURAT YUSUF** *Ina Makaru 12*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Alif Lam Raa. Hizi ni Aya za kitabu kinachobainisha (kila linalohitajiwa).

الٓرٰ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ﴿١﴾

2. Hakika Sisi tumeiteremsha Qurani kwa Kiarabu ili mupate kufahamu.

اِنَّآ اَنْزَلْنٰهُ قُرْءٰنًا عَرَبِيًّا لَّعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿٢﴾

3. Sisi tunakusimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qurani hii. Na hakika ulikuwa kabla ya haya ni miongoni mwa wasio na khabari (hizi).

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ اَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَآ اَوْحَيْنَآ
اِلَيْكَ هٰذَا الْقُرْاٰنَ ۖ وَاِنْ كُنْتَ مِنْ قَبْلِهٖ لَمِنَ
الْغٰفِلِيْنَ ﴿٣﴾

4. (Kumbusha) Yusufu alipomwambia baba yake: "Ewe babaangu! Hakika nimeona (katika ndoto) nyota kumi na moja na jua na mwezi. Nimeviona (vyote hivi) vikinisujudia."

اِذْ قَالَ يُوْسُفُ لِاَبِيْهِ يٰٓاَبَتِ اِنِّيْ رَاَيْتُ اَحَدَ عَشَرَ
كَوْكَبًا وَّالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَاَيْتُهُمْ لِيْ سٰجِدِيْنَ ﴿٤﴾

5. Akasema (babaake): "Ewe mwanangu! Usiwasimulie ndoto yako (hii) nduguzo wasije wakakufanyia vitimbi (kwa ajili ya husuda itakayowapanda). Hakika Shetani kwa mwanaadamu ni adui aliye dhahiri (atawatia uchungu tu)."

قَالَ يٰبُنَيَّ لَا تَقْصُصْ رُءْيَاكَ عَلٰٓى اِخْوَتِكَ
فَيَكِيْدُوْا لَكَ كَيْدًا ۗ اِنَّ الشَّيْطٰنَ لِلْاِنْسَانِ عَدُوٌّ
مُّبِيْنٌ ﴿٥﴾

6. "Namna hivi Mola wako atakuchagua na kukufundisha hakika ya mambo. Na atatimiza neema zake juu yako na juu ya kizazi cha Yaaqubu, (hao nduguzo na kizazi chao) kama alivyoitimiza zamani juu ya baba zako, Ibrahimu na Is-haqa. Bila shaka Mola wako ni Mjuzi na Mwenye hikima."

وَكَذٰلِكَ يَجْتَبِيْكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ
مِنْ تَاْوِيْلِ الْاَحَادِيْثِ وَيُتِمُّ نِعْمَتَهٗ عَلَيْكَ
وَعَلٰٓى اٰلِ يَعْقُوْبَ كَمَآ اَتَمَّهَا عَلٰٓى اَبَوَيْكَ مِنْ
قَبْلُ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْحٰقَ ۗ اِنَّ رَبَّكَ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٦﴾

7. Kwa yakini katika (kisa cha) Yusufu na ndugu zake yako mazingatio mengi kwa wanaouliza (mambo wapate kujua).

لَقَدْ كَانَ فِيْ يُوْسُفَ وَاِخْوَتِهٖٓ اٰيٰتٌ لِّلسَّآئِلِيْنَ ﴿٧﴾

---

2. Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 3 wamepindua tafsiri inayokubaliwa na wote; ya tamko hili *Arabiyyan*, yaani iliyoshuka kwa lugha ya Kiarabu. Wala hawapati mfasiri mmoja aliyeikataa tafsiri hii, isipokuwa wao; khalafu wanasingizia kamus la Lane na *Aqrabul Mawarid*. Na uwongo; hakusema huyo Lane wala mwenye Aqrab kuwa *Arabiyyan* iliyomo katika Aya hizi *Qur-anan Arabiyya* maana yake ni hizo mbili walizozitaja wao.

4. Unaonyeshwa hapa mwisho wa wema unavyokuwa na mwisho wa ubaya unavyomalizikia.

5. Mtu asiwe akisimulia tu bila haja — kila neema zake, kwani kila mwenye neema huhusudiwa na kutakiwa kudhuriwa.

8. (Kumbuka) waliposema (ndugu zake): "Hakika Yusufu na nduguye (yule aliye baba mmoja na mama mmoja naye) wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi, hali sisi (watoto wa mama wengine) ni kundi lenye nguvu, (na wao peke yao tu). Hakika baba yetu yumo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri, (hajui wenye nafuu naye na wasiokuwa na nafuu naye)."

إِذْ قَالُوا لَيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَىٰ أَبِينَا مِنَّا وَ
نَحْنُ عُصْبَةٌ ۚ إِنَّ أَبَانَا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾

9. "Muueni Yusufu au mtupeni nchi (za mbali) ili uso wa baba yenu ukuelekeeni (kwa kuwa wakati huo atakuwa hayuko huyo kipenzi chake); na baada ya haya mtakuwa watu wema (mtatubia kwa Mungu)."

اقْتُلُوا يُوسُفَ أَوِ اطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُ لَكُمْ وَجْهُ
أَبِيكُمْ وَتَكُونُوا مِن بَعْدِهِ قَوْمًا صَالِحِينَ ﴿٩﴾

10. Akasema msemaji katika wao: "Msimuue Yusufu, lakini mtupeni (mumueke) katika (jiwe la) ndani ya kisima kirefu, watamuokota baadhi ya wasafiri, kama nyinyi mna sharti ya kufanya kitu (cha kumbaidisha na baba yake)."

قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ لَا تَقْتُلُوا يُوسُفَ وَأَلْقُوهُ فِي
غَيَابَتِ الْجُبِّ يَلْتَقِطْهُ بَعْضُ السَّيَّارَةِ إِن
كُنتُمْ فَاعِلِينَ ﴿١٠﴾

11. (Baada ya kuwafikiana kwa shauri hii walikwenda kwa baba yao) Wakasema: "Ewe baba yetu Mbona hutuamini juu ya Yusufu; hakika sisi ni wenye kumtakia wema?"

قَالُوا يَا أَبَانَا مَا لَكَ لَا تَأْمَنَّا عَلَىٰ يُوسُفَ وَإِنَّا
لَهُ لَنَاصِحُونَ ﴿١١﴾

12. "Mpeleke kesho pamoja nasi (machungani); atakula kwa furaha na kucheza; na bila shaka sisi tutamlinda."

أَرْسِلْهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَعْ وَيَلْعَبْ وَإِنَّا لَهُ
لَحَافِظُونَ ﴿١٢﴾

13. (Baba yao) akasema: "Kwa hakika linanihuzunisha (mimi jambo hili la) nyinyi kwenda naye huko na ninaogopa (asije) mbwa mwitu akamla hali nyinyi mumeghafilika naye, (katika kazi zenu za uchungaji na nyinginezo)."

قَالَ إِنِّي لَيَحْزُنُنِي أَن تَذْهَبُوا بِهِ وَأَخَافُ أَن
يَأْكُلَهُ الذِّئْبُ وَأَنتُمْ عَنْهُ غَافِلُونَ ﴿١٣﴾

14. Wakasema: "Ikiwa mbwa mwitu atamla, na hali sisi ni kundi lenye nguvu kabisa, bila shaka tutakuwa wenye kukhasirika (tusiokuwa na maana)."

قَالُوا لَئِنْ أَكَلَهُ الذِّئْبُ وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّا
إِذًا لَّخَاسِرُونَ ﴿١٤﴾

15. Basi walipomchukua na wakakubaliana kumtia katika shimo la kisima kirefu, (walifanya hivyo). Na tukampa wahyi (Yusufu kwa kumtia Ilhamu katika moyo wake kuwa) "Utawaambia (baadaye) jambo lao hili (wanalokufanyia leo);" na hali wao (ndugu zake) hawatambui (kuwa anafunuliwa mambo hapo kisimani).

فَلَمَّا ذَهَبُوا بِهِ وَأَجْمَعُوا أَن يَجْعَلُوهُ فِي غَيَابَتِ
الْجُبِّ ۚ وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ لَتُنَبِّئَنَّهُم بِأَمْرِهِمْ هَٰذَا وَهُمْ
لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٥﴾

16. Wakaja kwa baba yao usiku wakilia.

وَجَاءُوا أَبَاهُمْ عِشَاءً يَبْكُونَ ﴿١٦﴾

9. Tamaa mbaya kabisa hiyo kusema 'Hebu nifanye maasi, khalafu nitatubia.' Maasi yakutokee tu hivi pasi na mwenyewe kuyatafuta, hapo ndipo Mwenyezi Mungu atakupokea bila ya shaka; utakapotubia kwake kwa maasi hayo; siyo kupanga tangu mwanzo kuwa 'Nitafanya hivi na hivi . . . kisha nitatubia.'

17. Wakasema: "Ewe baba yetu! Hakika tulikwenda kushindana mbio na tukamuacha Yusufu penye vyombo vyetu, basi mbwa mwitu akamla; lakini (wewe) hutatuamini (kwa haya tunayokwambia) ingawa tunasema kweli."

قَالُوا يَٰٓأَبَانَآ إِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ وَتَرَكْنَا يُوسُفَ
عِندَ مَتَٰعِنَا فَأَكَلَهُ ٱلذِّئْبُ ۖ وَمَآ أَنتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا
وَلَوْ كُنَّا صَٰدِقِينَ ﴿١٧﴾

18. Na wakaleta juu ya kanzu yake damu ya uwongo. (Baba yao) akasema: (alipoiona ile kanzu haikuchanika—walisahau kuichanachana): "Bali nafsi zenu zimekuzainishieni jambo (kumfanyia mwenzenu. Basi mumekwisha kufanya. Mumemuua kusudi) Basi (langu mimi ni) subira njema; na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayoyasema."

وَجَآءُو عَلَىٰ قَمِيصِهِۦ بِدَمٍ كَذِبٍ ۚ قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ
لَكُمْ أَنفُسُكُمْ أَمْرًا ۖ فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۖ وَٱللَّهُ ٱلْمُسْتَعَانُ
عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾

19. Ukafika msafara (karibu na pale kisimani) wakamtuma mteka maji wao, naye akatumbukiza ndoo yake (Kupanda ndoo ile akamwona mtoto) alisema: "Ee, furaha njema! Huyu hapa kijana mwanamume." Nao (yeye na wenziwe waliokuwa kisimani hapo) wakamficha (kwa wale wasafiri wenzao wakasema kuwa kijana huyo) ni bidhaa (waliyonunua). Na Mwenyezi Mungu akijua waliyokuwa wakiyafanya. (Wakenda naye Misri).

وَجَآءَتْ سَيَّارَةٌ فَأَرْسَلُوا وَارِدَهُمْ فَأَدْلَىٰ دَلْوَهُۥ ۖ قَالَ
يَٰبُشْرَىٰ هَٰذَا غُلَٰمٌ ۚ وَأَسَرُّوهُ بِضَٰعَةً ۚ وَٱللَّهُ عَلِيمٌۢ بِمَا
يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾

20. Na wakamuuza kwa thamani pungufu kwa pesa (kidogo tu hivi) za kuhisabika, na hawakuwa na haja naye (ya kumueka, wakiogopa wasitokee jamaa zake kuja kumtafuta huko).

وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍۭ بَخْسٍ دَرَٰهِمَ مَعْدُودَةٍ ۚ وَكَانُوا فِيهِ
مِنَ ٱلزَّٰهِدِينَ ﴿٢٠﴾

21. Na yule aliyemnunua huko Misri alimwambia mke wake: "Mtengenezee makazi ya hishima (mtumwa) huyu; hwenda akatufaa au tukampanga kuwa mtoto." Na kama hivyo tulimmakinisha (tulimkalisha) Yusufu katika nchi (ya Misri) kwa raha ili kumfundisha hakika ya (kila) maneno. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda juu ya jambo lake (alitakalo; lazima liwe); lakini watu wengi hawajui.

وَقَالَ ٱلَّذِى ٱشْتَرَىٰهُ مِن مِّصْرَ لِٱمْرَأَتِهِۦٓ أَكْرِمِى
مَثْوَىٰهُ عَسَىٰٓ أَن يَنفَعَنَآ أَوْ نَتَّخِذَهُۥ وَلَدًا ۚ
وَكَذَٰلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِى ٱلْأَرْضِ وَلِنُعَلِّمَهُۥ مِن
تَأْوِيلِ ٱلْأَحَادِيثِ ۚ وَٱللَّهُ غَالِبٌ عَلَىٰٓ أَمْرِهِۦ وَلَٰكِنَّ
أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢١﴾

22. Na (Yusufu) alipobaleghe tulimpa hukumu na ilimu. Na kama hivi tunawalipa wanaotenda mema.

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُۥٓ ءَاتَيْنَٰهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَكَذَٰلِكَ
نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾

---

19-20. Unaona kuuzana kulikuwako zaidi ya miaka 4000 kabla ya kuja dini ya Kiislamu aliyokuja nayo Nabii Muhammad; khalafu wakausingizia Uislamu kuwa ndio uliokuja na kuuza watu.

21-22. Inaonyeshwa namna gani wema unavyozaa wema.

24. Usimlipe uovu anaye — au aliyekufanyia — wema. Anayekufanyia huo uovu, na wewe usimfanyie, seuze asiyekufanyia, seuze anayekufanyia mema. Lakini kuna watu — ati wanajita Wana wa Adamu nao — ambao wanawafanyia uovu wanaowafanyia wema. Hao wanyama wamewashinda. Huwezi kulipa mema hutulii tu? Unalipa uovu. Hao ni majoka tu, na Mwenyezi Mungu atawasalitishia Inshallah mashaka.

23. Na (yule mwanamke) ambaye nyumbani mwake (Yusufu) alikuwamo, akamtamani (Yusufu) kinyume cha radhi yake (yeye Yusufu); na akafunga milango, na akamwambia, "Njoo." (Yusufu) akasema: "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu (na kufanya maasi). Hakika yeye (mumeo) ni bwana wangu, ametengeneza makazi yangu hapa vizuri (nyumbani mwake, sitamfanyia dhulma hii). Hakika madhalimu hawatengenekewi."

وَرَاوَدَتْهُ الَّتِي هُوَ فِي بَيْتِهَا عَنْ نَّفْسِهِ وَغَلَّقَتِ
الْأَبْوَابَ وَقَالَتْ هَيْتَ لَكَ ۚ قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ إِنَّهُ
رَبِّي أَحْسَنَ مَثْوَايَ ۖ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾

24. Na (mwanamke huyo) akamkazia nia (ya kutaka kumdhuru vile alivyomkataa) na (Yusufu) akamkazia nia (ya kumpiga; akitaka kumpiga). Kama (Yusufu) asingaliona dalili za (kufahamishwa na) Mola wake (kuwa kumpiga huyo mwanamke si uzuri, angelimpiga naye, bali alikimbia tu). Tumefanya namna hivi ili tumwepushie kila jambo la ubaya na la uovu (kama huko kuzini). Hakika yeye alikuwa katika waja wetu waliosafishwa.

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهِ ۖ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا أَنْ رَّأَىٰ بُرْهَانَ
رَبِّهِ ۚ كَذَٰلِكَ لِنَصْرِفَ عَنْهُ السُّوءَ وَالْفَحْشَاءَ ۚ
إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِينَ ﴿٢٤﴾

25. Na (wote wawili) wakakimbilia mlangoni (Yusufu ili akimbie), na mwanamke huyo akairarua kanzu yake kwa nyuma. Na wakamkuta mume wake mlangoni; mwanamke akasema (kumwambia mumewe katika kutia chonza za uwongo) "Hakuna malipo ya mwenye kutaka kufanya ubaya na mkeo isipokuwa kufungwa gerezani au kupewa adhabu inayoumiza." (Anamsingizia uwongo Nabii Yusufu kuwa anamtaka).

وَاسْتَبَقَا الْبَابَ وَقَدَّتْ قَمِيصَهُ مِنْ دُبُرٍ وَأَلْفَيَا
سَيِّدَهَا لَدَا الْبَابِ ۚ قَالَتْ مَا جَزَاءُ مَنْ أَرَادَ
بِأَهْلِكَ سُوءًا إِلَّا أَنْ يُسْجَنَ أَوْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٥﴾

26. (Yusufu) akasema: "Huyu (mwanamke) ndiye aliyenitaka bila mimi kumtaka." Na shahidi aliyekuwa katika jamaa za huyu (mwanamke) akatoa ushahidi (akasema): "Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele basi (mwanamke huyu) amesema kweli, naye (Yusufu) yu katika waongo."

قَالَ هِيَ رَاوَدَتْنِي عَنْ نَّفْسِي وَشَهِدَ شَاهِدٌ
مِّنْ أَهْلِهَا ۚ إِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدَّ مِنْ قُبُلٍ فَصَدَقَتْ
وَهُوَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٢٦﴾

27. "Na kama kanzu yake imechanwa nyuma, basi (mwanamke huyu) amesema uwongo, naye (Yusufu) yu katika wakweli."

وَإِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدَّ مِنْ دُبُرٍ فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ
الصَّادِقِينَ ﴿٢٧﴾

---

Na mambo ya kukaa mwanamume na mwanamke peke yao yamekatazwa kabisa katika Sharia kwani lazima yataleta mabaya. Wala usiseme "huyu shemeji yangu" — "ndugu wa mke wangu" au "shemeji yangu" — "mke wa ndugu yangu." Wote hao khatari kwako na kwao na walio kama hao. Faragha kitu kibaya kabisa.

21-27. Wajibu kwa mtu kukitakasa cheo chake kama ilivyo wajibu kuitakasa dini yake na kila chengine chake.

Hapa aliposingiziwa uwongo huo na bibi huyo, hakunyamaza; alibainisha lipi lililokuwa la kweli, bila ya kumonea haya huyo mwanamke aliyeondoa haya, akazidi kuazimia kufanya yaliyo mabaya.

Wala si lazima huyu 'Shahidi' kuwa alikuwa mtoto mdogo. Hapana shaka kuwa hiyo ni dalili madhubuti, akiisema mtoto mdogo au mtu mzima.

28. Basi (mumewe) alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma (alijua kuwa Yusufu ndiye aliyekuwa akitaka kukamatwa kwa nguvu) akasema: "Hakika hii ni katika hila zenu wanawake; bila shaka hila zenu ni kubwa. (Wewe ndiye uliyeazimia mabaya, unakwenda kumsingizia yeye!)"

فَلَمَّا رَءَا قَمِيصَهُۥ قُدَّ مِن دُبُرٍ قَالَ إِنَّهُۥ مِن كَيْدِكُنَّ ۖ إِنَّ كَيْدَكُنَّ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾

29. "Yusufu! Yaachilie mbali haya (usiyasimulie nje). Na wewe (mwanamke) omba msamaha kwa dhambi zako. Hakika wewe ni katika wanaofanya makosa."

يُوسُفُ أَعْرِضْ عَنْ هَٰذَا ۚ وَٱسْتَغْفِرِى لِذَنۢبِكِ ۖ إِنَّكِ كُنتِ مِنَ ٱلْخَاطِـِٔينَ ﴿٢٩﴾

30. Na wanawake wa mji ule (wakapata habari hii) wakawa wanasema: "Mkewe waziri anamtamani mtumishi wake pasi na kutamaniwa naye. Hakika amemuathiri kwa mapenzi. Bila shaka sisi tunamuona (mke wa waziri) yumo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

وَقَالَ نِسْوَةٌ فِى ٱلْمَدِينَةِ ٱمْرَأَتُ ٱلْعَزِيزِ تُرَٰوِدُ فَتَىٰهَا عَن نَّفْسِهِۦ ۖ قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا ۖ إِنَّا لَنَرَىٰهَا فِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾

31. Basi (mkewe waziri) aliposikia msemo wao huu aliwaita (waje wauone uzuri wa Yusufu wajue kuwa mwenye kurukwa na akili kwa kumpenda Yusufu hana lawama) na akawafanyia karamu na akampa kila mmoja katika wao kisu na akamwambia (Yusufu), "Tokeza mbele yao." Basi walipomuona waliona ni kitu kikubwa kabisa na wakakata mikono yao (kwa vile visu, na wenyewe hawana habari kwa kuwa wameshughulika kumtazama tu huyo Yusufu) na wakasema: "Hasha lillahi! Huyu si mwanaadamu; hakuwa huyu ila ni Malaika mtukufu."

فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ أَرْسَلَتْ إِلَيْهِنَّ وَأَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَّكَـًٔا وَءَاتَتْ كُلَّ وَٰحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّينًا وَقَالَتِ ٱخْرُجْ عَلَيْهِنَّ ۖ فَلَمَّا رَأَيْنَهُۥٓ أَكْبَرْنَهُۥ وَقَطَّعْنَ أَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَٰشَ لِلَّهِ مَا هَٰذَا بَشَرًا إِنْ هَٰذَآ إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿٣١﴾

32. (Mkewe waziri) akasema: "Huyu ndiye mliyenilaumia; na hakika nilimtamani kinyume cha nafsi yake, lakini akajilinda. Na kama hatafanya ninalomuamrisha, bila shaka (nitamfanyia kila vitimbi mpaka) atafungwa gerezani na atakuwa miongoni mwa madhalili (badala ya hii hishima anayoipata. Kisha wakaingia na wale wanawake nao kuwapeleka wajumbe kumtaka)."

قَالَتْ فَذَٰلِكُنَّ ٱلَّذِى لُمْتُنَّنِى فِيهِ ۖ وَلَقَدْ رَٰوَدتُّهُۥ عَن نَّفْسِهِۦ فَٱسْتَعْصَمَ ۖ وَلَئِن لَّمْ يَفْعَلْ مَآ ءَامُرُهُۥ لَيُسْجَنَنَّ وَلَيَكُونًا مِّنَ ٱلصَّٰغِرِينَ ﴿٣٢﴾

33. (Yusufu akasema: "Ee Mola wangu! Nastahabu zaidi gereza kuliko haya wanayoniitia; na usiponiondolea hila zao nitawaelekea na nitakuwa miongoni mwa wajinga (wafanyao maasi)."

قَالَ رَبِّ ٱلسِّجْنُ أَحَبُّ إِلَىَّ مِمَّا يَدْعُونَنِىٓ إِلَيْهِ ۖ وَإِلَّا تَصْرِفْ عَنِّى كَيْدَهُنَّ أَصْبُ إِلَيْهِنَّ وَأَكُن مِّنَ ٱلْجَٰهِلِينَ ﴿٣٣﴾

34. Basi Mola wake akapokea maombi (dua) yake na akamwondolea hila zao. Bila shaka Yeye ndiye anayesikia na ndiye anayejua.

فَٱسْتَجَابَ لَهُۥ رَبُّهُۥ فَصَرَفَ عَنْهُ كَيْدَهُنَّ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٣٤﴾

---

32. Tulitaja mbele kuwa kwa tamko la *Malakun Karym* wamekusudia wale wanawake kupiga mfano wa Sura nzuri, si Utakatifu. Nao Makadiyani wanajua, lakini wanapindua tu.

33. Wale wanawake baada ya kumuona Nabii Yusufu siku ile, walipandwa na mapenzi makubwa nao; ikawa wanampelekea mfululizo wajumbe na mabarua; akaona awe jela asalimike na wajumbe wao na barua zao na mengine yao. Kheri nusu ya shari kuliko shari kamili.

35. Kisha ikawadhihirikia (yule waziri na watu wake) baada ya kuona alama (zote za usafi wa Nabii Yusufu; iliwadhihirikia kuwa shauri bora la kumwondolea matusi yule mke wa waziri) ni kuwa wamfunge (yule Yusufu) kwa muda kidogo.

ثُمَّ بَدَا لَهُمْ مِّنْ بَعْدِ مَا رَاَوُا الْاٰيٰتِ لَيَسْجُنُنَّهٗ حَتّٰى حِيْنٍ ﴿٣٥﴾

36. Na wakaingia pamoja naye gerezani vijana wawili. Mmoja wao akasema: (kumwambia Nabii Yusufu): "Hakika nimejiona (katika ndoto) nakamua ulevi." Na mwingine akasema: "Hakika nimejiona (katika ndoto) nabeba mikate juu ya kichwa changu ambayo ndege wanaila. Tuambie tafsiri yake; kwa yakini sisi tunakuona wewe ni miongoni mwa watu wazuri."

وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيٰنِ ؕ قَالَ اَحَدُهُمَآ اِنِّيْٓ اَرٰىنِيْٓ اَعْصِرُ خَمْرًا ۚ وَقَالَ الْاٰخَرُ اِنِّيْٓ اَرٰىنِيْٓ اَحْمِلُ فَوْقَ رَاْسِيْ خُبْزًا تَاْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ ؕ نَبِّئْنَا بِتَاْوِيْلِهٖ ۚ اِنَّا نَرٰىكَ مِنَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٣٦﴾

37. (Yusufu) akasema: (Kwa Utume niliopewa Mimi naweza kukufasirieni ndoto zenu hizo na mambo mengine yaliyofichikana). "Hakitakujieni chakula cho chote mtakachopewa ila nitakwambieni tafsiri yake kabla hakijakujieni. (Mkitaka nitakufanyieni hivi mjue kuwa mimi Mtume). Hili ni katika yale aliyonifundisha Mola wangu. Hakika mimi sifuati mila ya watu wasiomuamini Mwenyezi Mungu, na wakawa hawaiamini Akhera."

قَالَ لَا يَاْتِيْكُمَا طَعَامٌ تُرْزَقٰنِهٖٓ اِلَّا نَبَّاْتُكُمَا بِتَاْوِيْلِهٖ قَبْلَ اَنْ يَّاْتِيَكُمَا ؕ ذٰلِكُمَا مِمَّا عَلَّمَنِيْ رَبِّيْ ؕ اِنِّيْ تَرَكْتُ مِلَّةَ قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿٣٧﴾

38. "Mimi nimefuata mila ya baba zangu, Ibrahimu na Is-haqa na Yaaqubu. Hatuna haki ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote. (Kujua) hivi ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yetu na juu ya watu (wengine); lakini watu wengi hawashukuru."

وَاتَّبَعْتُ مِلَّةَ اٰبَآءِيْٓ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ ؕ مَا كَانَ لَنَآ اَنْ نُّشْرِكَ بِاللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ ؕ ذٰلِكَ مِنْ فَضْلِ اللّٰهِ عَلَيْنَا وَعَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٣٨﴾

39. "Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je! Waungu wengi wanaofarikiana ndio bora (kuabudiwa) au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu (juu ya kila kitu?)"

يٰصَاحِبَيِ السِّجْنِ ءَاَرْبَابٌ مُّتَفَرِّقُوْنَ خَيْرٌ اَمِ اللّٰهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٣٩﴾

40. "Hamuabudu badala yake (Mwenyezi Mungu) ila majina (matupu) mliyoyapanga nyinyi wenyewe na baba zenu (mkayeta hayo masanamu). Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili kwa hayo. Haikuwa hukumu ila hii ya Mwenyezi Mungu tu; ameamrisha msimuabudu yoyote isipokuwa Yeye tu.

مَا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖٓ اِلَّآ اَسْمَآءً سَمَّيْتُمُوْهَآ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ مَّآ اَنْزَلَ اللّٰهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ؕ اِنِ الْحُكْمُ اِلَّا لِلّٰهِ ؕ اَمَرَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ ؕ ذٰلِكَ الدِّيْنُ الْقَيِّمُ

---

35. Yule waziri aliyemnunua Nabii Yusufu, mkewe akataka kufanya ubaya ule; alipoona linazidi kuwa baya jina la mkewe na kujaa ndimini mwa watu, aliona bora amfunge huyo Nabii Yusufu, ionekane kwa watu kuwa huyu ndiye aliyekuwa mbaya — si mkewe. Anataka kubabaisha kusudi.

36. Alipata Utume huko Jela akawa anawaambia watu mazuri na kuwafanyia mazuri. Kulikuwa na majeshi ya watu huko jela; wakapelekewa huyu Nabii Yusufu. Baadhi ya miujiza yake ilikuwa kutambua siri.

39-40. Anawabainishia baadhi ya Tawhidi ya Mwenyezi Mungu. Mtu huchukua fursa ya kufundisha popote pale anapopatia wasaa. Usitupe fursa ukiipata, usije ukajuta.

Hiyo ndiyo dini iliyonyoka, lakini watu wengi hawajui; (kama nyinyi hivi Mnaabudu masanamu, jua, wafalme wenu na kama haya. Sivyo hivi).

وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٠﴾

41. "Enyi wafungwa wenzangu wawili! Mmoja katika nyinyi (atarejezwa kazini kwake) akamnyweshe bwana wake ulevi (kama alivyokuwa akifanya zamani). Na ama yule mwingine atauawa kwa kusulubiwa, na ndege watamla kichwa chake. Limekwishakatwa (huko kwa Firauni) hili jambo mlilokuwa mkiuliza."

يٰصَاحِبَيِ السِّجْنِ اَمَّآ اَحَدُكُمَا فَيَسْقِيْ رَبَّهٗ خَمْرًا ۚ
وَاَمَّا الْاٰخَرُ فَيُصْلَبُ فَتَاْكُلُ الطَّيْرُ مِنْ رَّاْسِهٖ ۗ
قُضِيَ الْاَمْرُ الَّذِيْ فِيْهِ تَسْتَفْتِيٰنِ ﴿٤١﴾

42. Na (Yusufu) akamwambia yule aliyejua ya kwamba ataokoka katika wale wawili. "Unikumbuke mbele ya bwana wako (Firauni; umwambie kuwa nimeonewa nimefungwa bure)." Lakini Shetani alimsahaulisha kumkumbusha bwana wake. Kwa hivyo akakaa gerezani (Nabii Yusufu) baadhi ya miaka (baada ya hapa).

وَقَالَ لِلَّذِيْ ظَنَّ اَنَّهٗ نَاجٍ مِّنْهُمَا اذْكُرْنِيْ عِنْدَ رَبِّكَ ۡ
فَاَنْسٰىهُ الشَّيْطٰنُ ذِكْرَ رَبِّهٖ فَلَبِثَ فِي السِّجْنِ بِضْعَ
سِنِيْنَ ﴿٤٢﴾ ع ١٥

43. Na (siku moja) mfalme (Firauni aliota) akasema (kuwaambia mawaziri wake). "Hakika mimi nimeona (ndotoni) ng'ombe saba wanene wanaliwa na ng'ombe saba ving'onda. Na nimeona mashuke saba mabichi na mengine yaliyokauka. Enyi wakubwa! Niotoleeni ndoto yangu ikiwa nyinyi mnaweza kufasiri ndoto (kuotoa)."

وَقَالَ الْمَلِكُ اِنِّيْۤ اَرٰى سَبْعَ بَقَرٰتٍ سِمَانٍ
يَّاْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَّسَبْعَ سُنْۢبُلٰتٍ خُضْرٍ
وَّاُخَرَ يٰبِسٰتٍ ؕ يٰۤاَيُّهَا الْمَلَاُ اَفْتُوْنِيْ فِيْ رُءْيَايَ اِنْ
كُنْتُمْ لِلرُّءْيَا تَعْبُرُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Wakasema: "Ni ndoto zilizoparanganyika (hizo; si ndoto safi) wala sisi hatujui tafsiri ya ndoto hizi (zisizokuwa safi)."

قَالُوْۤا اَضْغَاثُ اَحْلَامٍ ۚ وَمَا نَحْنُ بِتَاْوِيْلِ
الْاَحْلَامِ بِعٰلِمِيْنَ ﴿٤٤﴾

45. Hapo akasema yule aliyeokoka katika wale (wafungwa) wawili, na akakumbuka (sasa maagizo ya Nabii Yusufu) baada ya muda (mrefu akasema): "Mimi nitakwambieni tafsiri yake. Basi nitumeni (nende nikakutafutieni tafsiri yake)."

وَقَالَ الَّذِيْ نَجَا مِنْهُمَا وَادَّكَرَ بَعْدَ اُمَّةٍ اَنَا
اُنَبِّئُكُمْ بِتَاْوِيْلِهٖ فَاَرْسِلُوْنِ ﴿٤٥﴾

46. (Akenda gerezani akamtaka msamaha Nabii Yusufu kwa kule kusahau kwake na akamwambia): "Yusufu! Ewe mkweli! Tueleze hakika ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba dhaifu. Na mashuke saba mabichi na mengine yaliyokauka, ili nirejee kwa watu wapate kujua."

يُوْسُفُ اَيُّهَا الصِّدِّيْقُ اَفْتِنَا فِيْ سَبْعِ بَقَرٰتٍ
سِمَانٍ يَّاْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَّسَبْعِ سُنْۢبُلٰتٍ
خُضْرٍ وَّاُخَرَ يٰبِسٰتٍ ۙ لَّعَلِّيْۤ اَرْجِعُ اِلَى النَّاسِ لَعَلَّهُمْ
يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٦﴾

---

41. Anawaagulia ndoto yao. Huyo atauawa kwa sababu alikitia sumu chakula cha mfalme kwa kutumwa na maadui zake. Ama makosa ya yule wa pili ni kuwa alikawia kumpa habari hii yule mfalme.

Wizi wa fadhila wa binaadamu umeanza zamani. Alipuza ule wasia wa rafiki yake ya kuwa amtaje kwa mfalme amwambie kuwa kuna Kijana mzuri amefungwa bure. Hata hili — alipopata huria yake — hakuweza kulikumbuka.

44. Ilivyowashinda tafsiri yake ndiyo wanajidai kuwa si ndoto iliyosafika hiyo — haifahamishi kitu.

قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَأَبًا ۚ فَمَا حَصَدْتُّمْ
فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلِهِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾

47. Akasema: "Mtalima myaka saba mfululizo kwa juhudi (yaani limeni miaka saba kwa juhudi kwani itaingia njaa kubwa baada ya myaka saba). Na mtakavyovivuna viacheni katika mashuke yake, isipokuwa kidogo mnavyokula (ili hivyo mnavyoviacha mule katika myaka ya njaa itakayokuja)."

ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَٰلِكَ سَبْعٌ شِدَادٌ يَأْكُلْنَ
مَا قَدَّمْتُمْ لَهُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تُحْصِنُونَ ﴿٤٨﴾

48. "Kisha itakuja baadaye myaka saba ya shida itakayokula vile mlivyoipa, (yaani watu watakula ile akiba mliyoiweka) isipokuwa kidogo mtakachohifadhi (kwa ajili ya kupandia)."

ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَٰلِكَ عَامٌ فِيهِ يُغَاثُ النَّاسُ وَ
فِيهِ يَعْصِرُونَ ﴿٤٩﴾ ع

49. "Kisha baada ya haya utakuja mwaka ambao katika mwaka huo watu watasaidiwa na (Mwenyezi Mungu); na katika huo watakamua (vya kukamua)."

وَقَالَ الْمَلِكُ ائْتُونِي بِهِ ۚ فَلَمَّا جَاءَهُ الرَّسُولُ
قَالَ ارْجِعْ إِلَىٰ رَبِّكَ فَسْئَلْهُ مَا بَالُ النِّسْوَةِ الَّتِي
قَطَّعْنَ أَيْدِيَهُنَّ ۚ إِنَّ رَبِّي بِكَيْدِهِنَّ عَلِيمٌ ﴿٥٠﴾

50. Na mfalme (alipopelekewa khabari hii) alisema: "Mleteni kwangu." Basi mjumbe (wa mfalme) alipomjia (Yusufu, alisema Yusufu) "Rudi kwa bwana wako ukamuulize khabari ya wanawake wale waliokata mikono yao; bila shaka Mola wangu anazijua sana hila zao (lakini nataka mfalme ajue usafi wangu ili anitakasie nia, asiniogope)."

قَالَ مَا خَطْبُكُنَّ إِذْ رَاوَدْتُّنَّ يُوسُفَ عَنْ نَّفْسِهِ ۚ
قُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ ۚ قَالَتِ امْرَاَتُ
الْعَزِيزِ الْـٰٔنَ حَصْحَصَ الْحَقُّ ۖ أَنَا رَاوَدْتُّهُ عَنْ نَّفْسِهِ
وَإِنَّهُ لَمِنَ الصّٰدِقِينَ ﴿٥١﴾

51. (Mfalme akawakusanya wale wanawake na akasema): "Nini jambo lenu lilikuwa mlipomtamani Yusufu kinyume cha matamanio yake?" Wakasema: "Hasha lillahi! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake (Tumejitahidi afanye mabaya na sisi, hakukubali kufanya)." Mkewe waziri (naye) akasema: "Sasa haki imedhihirika, mimi ndiye niliyemtamani kinyume cha nafsi yake, na bila shaka yeye yu miongoni mwa wakweli (kabisa)."

ذَٰلِكَ لِيَعْلَمَ أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ بِالْغَيْبِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي
كَيْدَ الْخَائِنِينَ ﴿٥٢﴾

52. (Na Yusufu akasema): "Hayo (ya kutaka waulizwe hivi) ni kwa sababu (waziri) ajue ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana nyuma yake; na ya kwamba Mwenyezi Mungu hazijaalii hila za makhaini kufanikiwa."

الجزء الثالث عشر (١٣)

وَمَا أُبَرِّئُ نَفْسِي ۚ إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ ۢ
بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۚ إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥٣﴾

53. Nami sijitakasi nafsi yangu; kwa hakika (kila) nafsi ni yenye kuamrisha sana maovu, isipokuwa ile ambayo Mola wangu ameirehemu. Hakika Mola wangu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

---

47. Hakumkasirikia akamwambia sikwambii usije ukapata ukubwa usiostahiki.

53. Ingawa inapasa mtu kukitakasa cheo chake lakini haipendezi kujisifu. Basi ndiyo hapa anabainisha kuwa haya aliyoyataka kwa mfalme ni kwa ajili ya kujitakasa asionekane kuwa mbaya na mwizi wa fadhila, sio kwa ajili ya kutaka kujionesha. Tarumbeta la kujipigia mtu mwenyewe halipendezi.

Na kule kujisifu kwake Nabii Yusufu katika Aya ya 55 ni kwa ajili ya dharura. Kwa ajili apewe yeye kazi ya